KATIBA

YA

THE CIVIC UNITED FRONT

(CUF-Chama Cha Wananchi)

KATIBA YA CHAMA 1992

(TOLEO LA 2014)

KATIBA

YA

THE CIVIC UNITED FRONT

(CUF – Chama Cha Wananchi)

KATIBA YA CHAMA 1992

(TOLEO LA 2014)

Toleo hili la nne tangu kutungwa kwa katiba hii ya THE CIVIC UNITED FRONT (CUF – Chama cha Wananchi) mwaka 1992 inajumuisha marekebisho yote yaliyofanywa hadi June 2014 na pia kutilia maanani maendeleo ya kisiasa ya Chama chetu na ya Tanzania kwa jumla kwa madhumuni ya kukiimarisha zaidi Chama chetu.

Mkutano Mkuu wa Taifa
June 2014

YALIYOMO

Kifungu Maelezo Ukurasa

UTANGULIZI 9

SURA YA KWANZA

JINA LA CHAMA, ALAMA, IMANI, NA MADHUMUNI YA CHAMA

1. Jina la Chama na Makao Makuu ya Chama 14
2. Bendera na alama nyingine za Chama 14
3. Nembo ya Chama 14
4. Wimbo wa Taifa 14
5. Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuanzisha alama nyengine 14
6. Imani ya Chama 15
7. Madhumuni ya Chama 16

SURA YA PILI

UANACHAMA, HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

SEHEMU YA KWANZA

8. Uanachama 20
9. Masharti ya uanachama 21
10. Kuacha na kuachishwa uanachama 21

SEHEMU YA PILI

11. Haki za mwanachama 22
12. Wajibu wa mwanachama 23

SURA YA TATU

MUUNDO, NGAZI, VIKAO NA VIONGOZI WA CHAMA

SEHEMU YA KWANZA

MUUNDO WA CHAMA

13. Muundo wa Chama 26
14. Maamuzi ya Chama 26

SEHEMU YA PILI

NGAZI YA TAWI

15. Tawi..... 27
16. Muundo wa Tawi 27
17. Mkutano Mkuu wa Tawi 27
18. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Tawi 27
19. Kamati ya Utendaji ya Tawi 29
20. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Tawi..... 29
21. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi 30
22. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi 31
23. Viongozi Wakuu wa Tawi 31
24. Kazi za Mwenyekiti wa Tawi..... 31
25. Kazi za Katibu wa Tawi 31
26. Kazi za Mweka Hazina wa Tawi 32
27. Kusimamishwa/kufukuzwa uongozi kwa Viongozi Wakuu wa Tawi 32
28. Mratibu wa Chama 33
29. Kazi za Mratibu wa Chama 33

SEHEMU YA TATU

NGAZI YA KATA

30. Kata na muundo wake..... 34
31. Mkutano Mkuu wa Kata 34
32. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Kata 35
33. Kamati ya Utendaji ya Kata..... 36
34. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata..... 36
35. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Kata 37

36. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata 38
37. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata 38
38. Viongozi Wakuu wa Kata 38
39. Kazi za Mwenyekiti wa Kata 39
40. Kazi za Katibu wa Kata 39
41. Kazi za Mweka Hazina wa Kata 40
42. Kusimamishwa/kufukuzwa uongozi kwa Viongozi Wakuu wa Kata 40

SEHEMU YA NNE

NGAZI YA JIMBO

43. Jimbo na muundo wake kwa Zanzibar na Tanzania Bara 41
44. Jimbo kwa Zanzibar 41
45. Mkutano Mkuu wa Jimbo na wajibu wake kwa Zanzibar 41
46. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Jimbo 42
47. Kamati ya Utendaji ya Jimbo 43
48. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo 43
49. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo 44
50. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo kwa Zanzibar 45
51. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo 46
52. Viongozi wakuu wa Jimbo kwa Zanzibar 46
53. Kazi za Mwenyekiti wa Jimbo 46
54. Kazi za Katibu wa jimbo 47
55. Kazi za Mweka Hazina wa Jimbo 47
56. Kuachishwa au kufukuzwa kwa Viongozi wakuu wa jimbo 48
57. Jimbo na Muundo wake kwa Tanzania Bara 48
58. Wajibu wa Kamati ya Utendaji wa Jimbo Tanzania Bara 49
59. Mwenyekiti na Katibu wa Jimbo 49
60. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tanzania Bara 49

SEHEMU YA TANO

NGAZI YA WILAYA

61. Wilaya na muundo wake 51
62. Mkutano Mkuu wa wilaya 51
63. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa wilaya 52
64. Kamati ya Utendaji ya Wilaya 54
65. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya wilaya 54
66. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya 57

67. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya 57
68. Vitengo vya Chama katika wilaya 57
69. Viongozi Wakuu wa wilaya 58
70. Kazi za Mwenyekiti wa wilaya 58
71. Kazi za Katibu wa wilaya 58
72. Miradi ya Vitengo 59
73. Kusimamishwa/Kufukuzwa uongozi kwa Viongozi Wakuu wa wilaya 59
74. Kusimamishwa/Kufukuzwa uongozi kwa Katibu wa wilaya 60

SEHEMU YA SITA

NGAZI YA TAIFA

75. Eneo la Chama Kitaifa 61
76. Muundo wa Chama Kitaifa 61
77. Mkutano Mkuu wa Taifa 61
78. Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa 62
79. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Taifa 63
80. Baraza Kuu la Uongozi la Taifa 66
81. Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa 66
82. Wajibu wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa 67
83. Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuchukua hatua za kinidhamu 69
84. Kamati ya Utendaji ya Taifa 70
85. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Taifa 71
86. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa 72
87. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa 73
88. Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa 73
89. Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa 74

SEHEMU YA SABA

VIONGOZI WA KITAIFA NA KAZI ZAO

90. Viongozi Wakuu wa Chama Kitaifa 75
91. Mwenyekiti wa Chama Taifa na kazi zake 75
92. Makamu Mwenyekiti wa Chama na kazi zake 77
93. Katibu Mkuu wa Chama na kazi zake 77
94. Kuachishwa/kufukuzwa uongozi kwa Viongozi Wakuu wa Chama Taifa 78
95. Naibu Katibu Mkuu wa Chama 79
96. Kazi za Naibu Katibu Mkuu 79
97. Kuachishwa/kufukuzwa uongozi kwa Naibu Katibu Mkuu 80

SURA YA NNE

BODI YA WADHAMINI, KAMATI, TAASISI NA KURUGENZI ZA CHAMA

98. Bodi ya Wadhamini 82
99. Kamati ya Maadili na nidhamu 82
100. Wajukumu ya Kamati ya Maadili na nidhamu 83
101. Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuanzisha Taasisi 83
102. Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuanzisha Kurugenzi 83
103. Jumuiya za Chama 84

SURA YA TANO

TARATIBU ZA UCHAGUZI KATIKA CHAMA

104. Uchaguzi wa Viongozi wa Chama 87

SURA YA SITA

MENGINEYO

105. Kukaimu Madaraka 89
106. Ofisi zilizoanzishwa 89
107. Fedha za Chama 89
108. Nidhamu ya Chama na muda wa kukata Rufaa 90
109. Chama kuelimisha wanachama 91
110. Kanuni za Chama 91
111. Lugha rasmi ya Chama 91
112. Kasma na uwezo wa madaraka 91
113. Masharti ya kuchaguliwa na kipindi cha Uongozi 93
114. Kuhalalisha kikao cha Chama 94
115. Uhalali wa maamuzi ya Chama 94
116. Mialiko kwa Wataalam 94
117. Kujiuzulu Uongozi 94
118. Uwezo wa kuunda Kamati za muda 95
119. Wabunge/Wawakilishi na Madiwani wa CUF 95
120. Wajibu wa kiongozi wa serikali wa Chama 95
121. Wabunge/Wawakilishi wa Chama kutunga kanuni 96
122. Mahudhurio ya kikao cha Chama 96
123. Ofisi za viongozi 96
124. Kujaza nafasi zilizowazi 96
125. Tafsiri ya maneno mbali mbali 96
126. Utekelezaji wa vifungu vya katiba 99
127. Jina la katiba na kuanza kutumika 99

UTANGULIZI

TAMKO LETU

BAADA YA KURUHUSIKA kuanzishwa kwa vyama vingi vya Siasa humu nchini Tanzania, mapema mwezi wa Julai, 1992.

SISI WATANZANIA WA PANDE ZOTE MBILI ZA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, TANZANIA BARA NA ZANZIBAR, tuliamua kukutana Mjini Dar-es-Salaam katika Ukumbi wa Starlight Hotel kama waasisi na kutafakari kwa kina na kuzingatia kwa uzalendo kuhusu maendeleo ya nchi yetu. Tuliangalia na kuchambua kwa undani namna maisha ya watu wetu yaliyokwishafikiwa katika kipindi cha miaka 28 ya Muungano wetu chini ya mfumo wa ukiritimba wa Siasa ya Chama kimoja.

TUMETAMBUA kuwa nchi yetu na watu wake mahala walipofikishwa hivi sasa, wataweza kunufaika zaidi kimaendeleo, kisiasa, kijamii na kitamaduni endapo wataikumbatia kikamilifu fursa pekee ya kihistoria iliyoanzishwa ya mfumo wa demokrasia ya kweli, yenye amani na utulivu katika maisha ya watu walio huru.

Tumegundua pia kuwa nchi yetu ni tajiri katika maliasili zilizomo ardhini, majini na hewani. Maliasili hizi zinaweza kutumiwa kwa manufaa na maslahi ya wananchi wote, juhudi ya kila mmoja wetu aliyeko mjini na kijijini, aliyeko shambani na kazini maadamu tu taifa na vyombo vyake, vinaheshimu na kulinda demokrasia na haki za Binadaamu na haki za watu kama zilivyotangazwa na Umoja wa Mataifa(UN) na Umoja wa Nchi za Afrika (AU).

KWA KUWA: Sisi Watanzania tuliokutana Dar es Salaam kwa muda wa siku mbili,tarehe 20 – 21 Novemba 1992 tunaamini kuwa Haki za Binadamu na Haki za Watu, kama zilivyotangazwa katika Tangazo la Haki za Binadaamu la Umoja wa Mataifa, na HATI ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika juu ya Haki za Binaadamu na Haki za Watu, ndiyo msingi wa Sheria na Kanuni zinazotakiwa kuongoza nchi;

KWA KUWA: Sisi Watanzania tuliokutana Dar es Salaam kwa muda wa siku mbili,tarehe 20 – 21 Novemba 1992 tunaamini kuwa

Haki za Binadamu na Haki za Watu, kama zilivyotangazwa katika Tangazo la Haki za Binadaamu la Umoja wa Mataifa, na HATI ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika juu ya Haki za Binaadamu na Haki za Watu, ndiyo msingi wa Sheria na Kanuni zinazotakiwa kuongoza nchi;
Tunaamini kwamba kwa kufuatana na imani yetu ya Haki za Binadaamu na Haki za Watu, wanawake wana haki ya kushiriki katika maamuzi yanayohusu maisha yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii bila ubaguzi kwa misingi ya jinsia au mila;

HIVYO BASI TUNATAMKA KWAMBA:

"Sisi tuliokutana Dar-es-Salaam tarehe 20 mpaka tarehe 21 Novemba 1992 tumeamua kuunda Chama cha Siasa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kitakachoitwa:

THE CIVIC UNITED FRONT (CUF – Chama Cha Wananchi)

Tumeamua kuunda Chama hiki **THE CIVIC UNITED FRONT (CUF – Chama Cha Wananchi)** kwa nia ya kuwaunganisha watu wa Tanzania wenye kuamini kwa dhati kuwepo kwa demokrasia ya kweli ambapo wananchi wenyewe ndio wenye mamlaka, madaraka na uamuzi wa mwisho kuhusu mambo yao na ya nchi yao.

Tumechukua uamuzi huo wa kihistoria ili kutekeleza imani yetu juu ya Haki za Binadaamu na Haki za Watu, kwa kutumia Itikadi, au falsafa yetu mpya itakayojulikana kwa jina la **ULIBERALI,** yenye maana pana ya *Haki Sawa Kwa Wote na Neema kwa Wote.*

NA KWA HIVYO:

(i) Tunasisitiza kuwa ni jukumu la Chama chetu, pale kitakapopata imani za wananchi walio wengi, kujenga nchi yetu upya kwa kuthamini ubinadamu, utu wa mtu binafsi, na nafasi ya kila mtu, kazi, uzoefu wake, ujuzi wake, ubunifu wake, elimu yake na juhudi yake kama mwananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutumia **UTAJIRI** wa maliasili ya nchi yetu, iliyopo angani, nchi kavu na baharini, ili kutekeleza Sera ya Chama ya Ustawi wa Maendeleo ya kila Mtanzania wa Bara na wa Zanzibar, katika ukamilifu wa nafsi yake kiroho, kiakili, kimwili, kitabia na kijamii.

Utekelezaji huo ambao utazingatia kwa namna gani Watanzania wote watajenga na kuimarisha ushirikiano mwema wa wote wale wanaopigania haki katika nchi yetu na katika nchi za kiafrika na za ulimwengu ambamo bado haki za binaadamu na haki za watu zinapuuzwa na kuvunjwa.

(ii) Tunasisitiza kwa wanachama wenzetu kuwa, kazi kubwa ya chama hiki itakuwa kushirikisha upya jamii ya Watanzania iliyozindukana, jamii ambayo iko vijijini na mijini, ili itende wajibu wao wa kuiletea Tanzania maendeleo zaidi, maendeleo ya kweli na yenye ustawi, kwa kuviongoza vyombo na Taasisi za dola katika kuhakikisha kuwa zinatoa haki sawa kwa wananchi wote, na kukwepa uonevu,unyanyasaji na ukandamizaji wa aina zote, ikiwa ni pamoja na ukiritimba wa mawazo.

(iii) Lengo hili litafanikiwa tu kwa kuupa fursa na uhuru kamili umma na jamii iliyozindukana kwa jumla, pamoja na watu binafsi waliozindukana, waweze kubuni njia za kiuchumi zenye urari wenye tija, na ambazo zitaleta maendeleo yenye maslahi yao ili kuimarisha amani ya kweli, itokanayo na uchumi imara utakaowanufaisha kwa haki wananchi wote, kwa nia ya kuwatoa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika umasikini na ufukara wa kutupwa na wakujitakia na badala yake kuifikisha nchi katika enzi ya **NEEMA** kwa wote.

(iv) Hali kadhalika Katiba hii ya Chama hiki pamoja na Kanuni zake zimetungwa kwa kuzingatia Katiba zote za nchi yetu. Pia, Katiba hii imezingatia kwa makini masharti muhimu ya vifungu vya sheria Na. 5 ya 1992 inayohusu USAJILI WA VYAMA VYA SIASA TANZANIA. Hivyo basi Katiba hii ina madhumuni ya kulinda, kuendeleza na kustawisha umoja wa Taifa, amani, utulivu, mshikamano na mashirikiano kwa kung'ang'ania kutekelezwa masharti ya demokrasia ya kweli katika shughuli zote za dola na za umma, ili kufikia malengo yetu ya kuunda Chama cha kitaifa kwa misingi tuliyoieleza hapo juu.

SISI WAASISI WA CHAMA HIKI

Tunaazimia kuweka misingi ya kufanya maamuzi yetu kwa njia za amani, kidemokrasia, kuheshimiana, na kuheshimu taratibu zitakazoandikwa na Katiba hii na Kanuni zitakazokuwa zikitungwa mara kwa mara; na daima tutatumia utaratibu mzuri wenye heshima katika kuwashirikisha wananchi wenzetu kuunga mkono Chama chetu, Itikadi yetu ya ULIBERLI na Sera zake.

KWA HIYO

Tunasisitiza kwa kila mwananchi atayejiunga na Chama hiki akumbuke kuwa amani ni kichocheo cha maendeleo na utamaduni wa Chama chetu.

Mkutano Mkuu wa Kwanza Wa Waasisi wa Chama

Novemba 20 – 21, 1992

Starlight Hotel

Dar-es-Salaam.

SURA YA KWANZA

JINA, ALAMA, IMANI NA MADHUMUNI YA CHAMA

Jina la Chama

1. (1) Chama hiki kitajulikana kwa jina la THE CIVIC UNITED FRONT (CUF – Chama Cha Wananchi) na kwa kifupi **"CUF"**

(2) Makao Makuuu ya Chama yatakuwa katika Mji Mkuu wa Zanzibar na anuani yake itakuwa kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(3) Kutakuwa na Ofisi Kuu ya Makao Makuu ya Chama Mjini Dar es Salaam na anuani yake itakuwa kama itakavyoamuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Bendera na alama nyingine za Chama

2. Chama kitakuwa na bendera kama ilivyowekwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba hii. Bendera ya Chama itakuwa kitambaa cha mji wa rangi nyeupe, katikati ya bendera kutakuwa na nembo ya Chama ambapo juu ya nembo hiyo kutakuwa na neno "CUF". Ukingoni mwa mji wa rangi nyeupe utazungukwa na fito za rangi ya bluu iliyopauka,nyekundu na bluu nyingine iliyopauka ambapo:

a) Rangi nyeupe ya mji wa bendera ya Chama inamaanisha amani na nia njema ya Chama ya kuendeleza amani ndani na nje ya Nchi yetu.

b) Rangi bluu katika ufito wa pembezoni ina lengo la kuunga mkono tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu na Tamko la Nchi za Umoja wa Afrika la Haki za Binadamu na Haki za Watu.

c) Rangi nyekundu katika ufito huo wa pembezoni inaonyesha harakati na jitihada zilizofanywa na wanachama wa Chama hiki kufikia mfumo wa demokrasia wa vyama vingi vya siasa nchini Tanzania

Nembo za Chama

3. Kutakuwa na nembo ya chama ambayo itakuwa na alama zifuatazo:-

a) Nuru itayomaanisha ukweli na matumaini mema.
b) Mizani itayomaanisha azma ya chama ya kusimamia utoaji wa haki sawa kwa wote.
c) Mikono iliyoshikana inayoonesha udugu, umoja na mashirikiano miongoni mwa wananchi wote wa nchi yetu

Wimbo wa Taifa wa Chama

4. (1) Kutakuwa na Wimbo wa Taifa wa Chama kama ulivyoelezwa katika nyongeza ya pili ya Katiba hii.

(2) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kurekebisha au kubadilisha wimbo wa Taifa wa chama.

Baraza Kuu kuanzisha alama nyingine

5. (1) Baraza Kuu la Uogozi la Taifa linaweza kuanzisha alama nyengine yoyote ile ya Chama ambayo Baraza litahisi alama hio inafaa kwa maslahi ya Chama.

(2) Bendera, nembo, wimbo wa Taifa wa Chama au alama nyingine yeyote ya Chama itaweza kutumika pahala popote au sehemu yeyote ile ambayo Kamati ya Utendaji ya Taifa itaelekeza.

Imani ya Chama

6. (1) Chama kinaamini kwamba:-

a) Binadamu ni mtu aliyeumbwa huru mwenye haki na uwezo wa kujiendeleza hadi upeo wake.

b) Utu wa binadamu hautagandamizwa wala kudumazwa na mtu yeyote au kundi lolote la watu kwa misingi ya rangi, kabila, dini, siasa, utaifa, mila au jinsia.

c) Binadamu wote wanastahili kupewa fursa na haki sawa ya kujiendeleza katika nyanja zote za kimaisha iwe katika kuishi kwa furaha katika familia, ulinzi na hifadhi ya sheria, elimu, afya, kumiliki mali halali, utamaduni na michezo na uongozi katika jamii kwa madhumuni ya kuhakikisha heshima ya utu kwa wote.

d) Maendeleo halisi ya binadamu hutokana na utu wake, uhuru na haki na yote hayo hudumishwa katika nchi inayofuata demokrasia, katiba, sheria za nchi na itikadi iliyo nzuri kama ya Uliberali.

e) Mipango ya maendeleo hutokana na maamuzi ya wananchi wenyewe, na huu ndio msingi wa mantiki ya itikadi na falsafa ya Uliberali.

f) Binadamu anao pia wajibu wa kutunza mazingira yake vizuri na kustawisha ulimwengu anamoishi.

g) Kila mtu ana wajibu wa kuheshimu utu, uhuru, na haki za wengine pamoja na kutii sheria zote za nchi.

(1) Pale ambapo pana sababu muhimu za Kitaifa, kama vile vita, maafa makubwa na kadhalika, kwa misingi ya imani ya chama, mwanachama atatakiwa kusalimisha kwa Taifa baadhi ya uhuru na haki zake za kibinadamu mradi tu iwe kwa kufanya hivyo heshima na utu wake utazingatiwa na kulindwa na dola, na serikali iliyopo madarakani.

(3) Serikali na taasisi za kutunga sheria daima zitabaki kuwa ni vyombo vinavyowekwa na wananchi ili kulinda haki za watu wote.

(4) Mahakama za nchi lazima ziwe huru na kuweza kuamua mambo yote yanayowekwa mbele yao kwa mujibu wa sheria za nchi na bila kuingiliwa na mtu au chombo kingine chochote isipokuwa kwa njia za rufaa kwa mahakama za juu yao.

(5) Utawala wa sheria na mahakama huru ndiyo ngao kubwa ya demokrasia ya nchi yetu

7. Lengo na madhumuni ya Chama ni:-

Madhumuni ya Chama

(1) Kuwaunganisha Watanzania ili wakatae uonevu, kudhalilishwa, kunyanyaswa, kubaguliwa au maovu mengine yanayoweza kufanywa dhidi ya heshima ya utu wa binadaamu, yawe yanayotendwa na Serikali, kikundi cha watu walio na uwezo kwa ajili ya mabavu yao au kwa ajili ya kujinufaisha kwao kiuchumi au kisiasa na kiitikadi au kwa kujali dini, kabila, jinsia au rangi zao.

(2) Kulinda na kuendeleza haki za binadamu kama zilivyotamkwa katika matangazo makuu ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi huru za Afrika, na kulinda taasisi zitakazohakikisha kwamba haki hizo zinaheshimiwa na zinatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

(3) Kudumisha, kulinda na kustawisha demokrasia kwa kuhakikisha kwamba wananchi wote wana haki na fursa sawa ya kuchagua viongozi wa siasa wa kuendesha serikali yao wakiwemo Rais, Wabunge,Wawakilishi, Madiwani viongozi wa serikali za vitongoji, vijiji na mitaa, na wajumbe wa vyombo vyote vitakavyowekwa na wananchi wenyewe moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi wao.

(4) Kuhakikisha kwamba wananchi wana madaraka ya kujiamulia wenyewe masuala yote ya maendeleo yao kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni na hivyo kuondoa mtindo wa kupangiwa na wajanja wachache wenye ukiritimba wa wazi na uroho wa madaraka au mali wanazotaka kuzipata kwa njia zisizokuwa za halali

(5) Kuondoa mambo yote yanayoruhusu rushwa, ufisadi, ubadhirifu, uonevu, ukandamizaji na ubaguzi wa aina yeyote.

(6) Kufanikisha itikadi ya Uliberali kwa kumlenga mtu mmoja mmoja, kikundi chenye malengo yanayofanana, na jamii kwa jumla, kwa minajili ya kuwaendeleza kikamilifu, kiroho, kiakili, kimwili, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

(7) Kuhakikisha kwamba siasa inatumikia uchumi badala ya uchumi kutumikia siasa.

(8) Kushika hatamu za dola kupitia ridhaa za wananchi, ili dola au serikali itekeleze vizuri itikadi na sera za Chama na ustawi wa Taifa letu.

(9) Kuhakikisha na kudumisha uhuru wa Mahakama pamoja na uhuru wa Bunge na Baraza la Wawakilishi na kwa kuzingatia vilivyo mgawanyo wa madaraka baina ya Utawala, Bunge au Baraza la Wawakilishi, na Mahakama kwa lengo la kumtendea haki sawa kila mwananchi na mtu mwingine yeyote.

(10) Kushirikiana na vyama vingine vya siasa humu nchini, katika kudumisha uhuru wa Taifa, amani ya nchi, na udugu wa asili wa Watanzania uliokwisha shamiri pamoja na kuleta maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii nchini kote.

(11) Kufanya juhudi za kukuza ushirikiano wa nchi za Afrika ya Mashariki na nchi nyingine za Afrika zenye kupenda amani na demokrasia. CUF itatumia nguvu za umoja na uhuru wa Watanzania kama nyenzo za kujenga ushirikiano huo katika Afrika.

(12) Kulinda na kuendeleza haki za wanawake, wazee wasiojiweza, walemavu na watoto kwa kuondoa hali yoyote ile inayowapuuza, inayowadhalilisha na inayowaonea.

(13) Kusikiliza na kuzingatia maoni ya kila mtu au makundi ya watu yenye manufaa kwa Taifa.

(14) Kuwalinda na kuwatunza wasiojiweza kama vile walemavu, wazee, mayatima, wastaafu, wananchi wanaokumbwa na maafa na majanga au wale wanaopuuzwa na dola yao hasa wakati wa majanga makubwa.

(15) Kushirikiana na mataifa mengine na vyama vingine vya siasa au visivyokuwa vya siasa, iwe vya kitaifa na, au vya kimataifa katika kudumisha usalama na amani, kuwaletea wananchi maendeleo na katika kulinda na kuhifadhi maliasili na mazingira yetu na ya ulimwengu.

(16) Kujenga uchumi wa taifa ulio imara na unaojitegemea kwa kiwango kikubwa na kulitoa Taifa la Tanzania kwenye umasikini na ufukara wa kujitakia na badala yake kulielekeza taifa kwenye neema yenye manufaa kwa wote kwa kutekeleza sera zitokanazo na itikadi sahihi ya Uliberali.

(17) Kushirikiana na vyama vingine vya siasa vya nchi marafiki ambavyo malengo yao, madhumuni yao, sera na itikadi zao zinakubaliana na malengo, madhumuni, sera na itikadi za chama hiki.

(18) Kujenga nchi isiyo na vitisho, isiyo na uonevu wa aina yoyote ile na isiyo na fujo. CUF itawalinda wananchi wote dhidi ya uonevu unaoweza kutendwa na vyombo vya dola visivyoongozwa kwa uadilifu. CUF inadhamiria kujenga utamaduni wa kuaminiana na kuheshimiana ili kulinda usalama wa raia na mali zao.

(19) Kuwaomba Watanzania wote, wakati wowote ule na bila kujali asili zao, dini zao, itikadi zao za kisiasa au nafasi zao katika jamii, kuiunga mkono CUF pamoja na kuiamini na pia kuwaamini viongozi wa Chama hiki.

(20) Kuunda serikali itakayojali maisha ya watu wote. Serikali ya CUF haitotumia madaraka vibaya kwa ajili ya kuwanufaisha viongozi wachache kwa kujikusanyia utajiri kwa njia zisizokuwa za halali.

(21) Kupiga vita ukandamizaji wa raia katika nyanja za uchumi, siasa na maendeleo ya kijamii, kuheshimu utu wa kila mtu, uhuru wa kila mwananchi, haki za binadamu pamoja na kuhakikisha kuwa hakuna dhuluma inayofanywa na mtu au chombo chochote kwa kukiuka utawala wa sheria kwa lengo la kuleta amani na utulivu wa kudumu.

SURA YA PILI

UANACHAMA, HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

SEHEMU YA KWANZA

UANACHAMA

Uanachama

8. (1) Mtu yeyote yule:

(a) Ambaye ni raia wa Tanzania, na

(b) Ambaye amefikia umri wa miaka 18 au zaidi,na

(c) Ambaye anakubaliana na madhumuni, imani, itikadi na sera za Chama, na

(d) ambaye si mwanachama wa chama kingine cha siasa anaweza kuomba kujiunga na Chama hiki na ikiwa atakubaliwa na vikao vinavyohusika, atakuwa ni mwanachama wa Chama hiki.

(2) Mtu yeyote anayeomba kuwa mwanachama:-

(a) Atajaza fomu ya maombi na kuiwasilisha kwenye tawi lililoko katika eneo lake.

(b) Ataorodheshwa katika daftari la wanachama la tawi hilo pindi ikiwa amekubaliwa.

(c) Mara baada ya kukubaliwa ombi lake atalipa kiingilio na kupewa haki ya uanachama na baadaye atalipa ada ya kila mwezi kama zitakavyoamuliwa mara kwa mara na Baraza Kuu la Uongozi laTaifa la Chama.

(3) Mtu yeyote aliyeomba kuwa mwanachama na akakataliwa anaweza kuomba tena baada ya kipindi cha miezi sita kupita na akikataliwa mara ya pili, ataweza kukata rufaa kwenye ngazi ya Kata au Jimbo ambalo tawi lake limo, na kama atakataliwa ataweza kukata rufaa kwenye ngazi ya wilaya kwa uamuzi wa mwisho.

(4) Mamlaka yote ya kuingiza mwanachama mpya katika chama hiki yako chini ya tawi ambalo mwanachama huyo anaishi au ameomba kuwa mwanachama wa tawi hilo

(5) Pale ambapo kiongozi wa Chama au wa serikali atokanaye na Chama atafanya mkutano wa hadhara na ikiwa katika mkutano huo pana mtu au watu wanaotaka kujiunga na Chama papo hapo, basi kiongozi huyo anaweza, bila kuathiri masharti ya kijifungu cha (4) cha kifungu hiki, kumpokea mtu huyo au kuwapokea watu hao, kuwa mwanachama mpya au wanachama wapya wa Chama hiki.

(6) Mwanachama aliyepata uanachama chini ya masharti ya kijifungu cha (5) cha kifungu hiki, mara baada ya mkutano wa hadhara kumalizika, na si zaidi ya mwezi mmoja kuanzia tarehe ya ulipofanyika mkutano huo, atatakiwa kukamilisha matakwa yote ya Katiba kama yalivyoainishwa katika kifungu cha 8(2)(a),(b) na (c) cha Katiba hii.

Masharti ya uanachama

9. Mtu yeyote atakayekubali kuingia katika Chama au kuendelea kuwa mwanachama atatakiwa atimize masharti yafuatayo na yale ambayo mara kwa mara yatawekwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au chombo kingine chochote cha Chama chenye mamlaka hayo:-

(1) Awe ni mtu anayelinda na kuitetea Katiba ya Chama na Kanuni zake pamoja na kuzieneza, kuzisimamia na kuitekeleza Itikadi ya ULIBERALI, sera, programu, Ilani na mikakati ya Chama itakayopitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa mara kwa mara .

(2) Awe ni mtu mwenye kujiheshimu na kuheshimu watu wengine na uhuru wao, maoni na mawazo yao, haki zao za kibinadamu, serikali halali za nchi, Bunge au Baraza la Wawakilishi, mamlaka nyengine za utawala, pamoja na mahakama zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba za nchi.

(1) Awe mtiifu kwa Chama, na anayeheshimu taratibu na maamuzi halali ya Chama

(3) Awe ni mtu anayependa mashirikiano na wenzake,

(4) Awe ni mtu mwenye uchu wa kuleta maendeleo nchini.

Kuacha na kuachishwa uanachama

10. (1) Mwanachama yeyote atasita kuwa mwanachama ikiwa:-

a) Atajiuzulu mwenyewe, au
b) Atafukuzwa au kuachishwa uanachama na tawi lake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, au
c) Atafukuzwa au kuachishwa uanachama na Mkutano Mkuu wa Taifa au Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, au
d) Atasita kulipa ada kwa kipindi cha mwaka mmoja mfululizo,au
e) Atashindwa kuheshimu Katiba ya Chama au kutoheshimu masharti ya uanachama, au
f) Atachukua uraia wa nchi nyingine, au
g) Atakuwa mwanachama wa chama kingine cha siasa.

(2) Mtu yeyote aliyeacha uanachama chini ya kifungu 10(1) (b),(c),(d) au (e) ataweza kukata rufaa kwa ngazi ya juu yake, ila ijulikane tu kwa wale waliofukuzwa au waliothibitishwa kufukuzwa kwao na Mkutano Mkuu wa Taifa basi hakuna chombo chochote katika Chama kitakachozungumzia uamuzi huo.

(3) Mtu yeyote anayepoteza uanachama wake chini ya kifungu 10(1) atapoteza haki zake zote za uanachama na hatorudishiwa ada, zawadi, au ruzuku yoyote aliyokwisha itoa kabla ya kupoteza uanachama huo.

(4) Uwezo wa kumuachisha uanachama mwanachama yeyote wa kawaida au kiongozi wa Chama wa Tawi umo mikononi mwa Tawi lake na au Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(5) Mwanachama yeyote ambaye ana wadhifa katika Chama au serikali(kiongozi kwa tiketi ya Chama) anaweza kuachishwa au kufukuzwa uanachama na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au Mkutano Mkuu wa Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(6) Mwanachama yeyote aliyefukuzwa, kuachishwa au kujiuzulu uanachama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii hatoweza kugombea nafasi ya uongozi wowote ule wa Chama au serikali kupitia Chama mpaka ipite miaka miwili kuanzia siku aliyofukuzwa au aliyojiuzulu au aliyoachishwa.

(7) Mwanachama yeyote aliyeachishwa au aliyefukuzwa uanachama anaweza kujiunga tena na Chama baada ya kupindukia miaka miwili tokea aachishwe ikiwa atapeleka maombi yake kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na kukubaliwa.

SEHEMU YA PILI

HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

11. Kila mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:-

Haki za Mwanachama

(1) Kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli zote za Chama zinazomuhusu.

(3) Kuhudhuria, kushiriki katika mijadala ya vikao vya Chama na kupiga kura pale anapohusika katika vikao vinavyomhusu ambavyo yeye ni mjumbe wake.

(4) Kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi, ujumbe au uwakilishi wa Chama, au serikali kwa kupitia Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na Kanuni zilizowekwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa la Chama kwa ajili ya uchaguzi.

(5) Kuonana na kiongozi yeyote wa Chama kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

(6) Kujitetea mbele ya chombo chochote cha Chama kinachotaka kumchukulia hatua za nidhamu dhidi yake, na kuomba kukata rufaa hadi kufikia ngazi ya mwisho, isipokuwa pale ambapo Katiba hii inaeleza vyenginevyo, ikiwa hataridhishwa na uamuzi uliokwishatolewa. Taarifa ya kukata rufaa inabidi itolewe na muhusika ndani ya siku 14 tangu mwanachama huyo kuchukuliwa hatua au rufaa yake kukataliwa, na rufaa hiyo isikilizwe katika kikao chochote kinachofuatia cha ngazi inayohusika.

(7) Kumkosoa kiongozi, mwanachama au mfanyakazi wa Chama kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

12. Kila mwanachama atakuwa ana wajibu ufuatao:-

Wajibu wa Mwanachama

(1) Kuisoma, kuifahamu, na kuiheshimu Katiba hii na kuyatekeleza masharti yake yote, ikiwa ni pamoja na Kanuni zitazotungwa mara kwa mara na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuidhinishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(2) Kuijua, kuikubali, kuilinda na kuitetea imani ya Chama pamoja na madhumuni yake.

(3) Kuyafahamu malengo ya Chama na kuyaunga mkono na kuyatetea.

(4) Kukieneza Chama kwa kuwashawishi wananchi kujiunga na Chama kwa kuzieneza sera za Chama kwa kadiri ya uwezo wake wote.

(5) Kukiunga mkono Chama kwa kuwapigia kura wanachama waliowekwa na Chama kwa ajili ya kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi wa nchi utakaohusisha vyama vingine vya siasa.

(6) Kulinda heshima ya Chama kwa kuwa na tabia njema, kutekeleza masharti ya Katiba ya Chama, kutii kanuni za Chama, kutii sheria na sheria ndogo ndogo za serikali iliyoundwa kihalali na pia, kwa busara, kukosoa utekelezaji mbaya wa serikali kwa hoja za msingi ili kuendeleza maslahi ya Chama, masilahi yake mwenyewe, masilahi ya wanachama wenzake, masilahi ya nchi na masilahi ya raia wote wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania.

(7) Kuwa mwaminifu kwa Chama na Serikali zilizoundwa kihalali na kwa ridhaa ya wananchi na kuwa tayari kuwatumikia watu kwa juhudi, maarifa, na vipaji vyake vyote.

(8) Kuhudhuria vikao vya Chama vinavyomuhusu na vile alivyoalikwa kwa barua, simu, fax, e-mail au kwa ujumbe wa ofisa wa Chama.

(9) Kuimarisha umoja na kujenga mapenzi baina ya wananchi kwa kuwa raia mwema, kuwaheshimu watu na kuwasaidia wasiojiweza, wazee na watoto kila inapowezekana.

(10) Kuwa tayari kupambana na namna yoyote ya uonevu, ukandamizaji, udhalilishaji na ubaguzi.

(11) Kujielimisha zaidi ili aweze kukabiliana na dhamana zote atakazopewa na Chama au dola ili azitekeleze vyema kwa maslahi ya wanachama na wananchi wote wa Tanzania.

(12) Kulinda kutetea haki za binadamu na haki za watu nchini na popote duniani pale mwananchi yeyote anapoonewa au kudhalilishwa, au kudhulumiwa na dola au serikali ya ngazi yoyote ile iliyoko madarakani.

(13) Kutumia uhuru na haki zake bila ya kuingilia uhuru na haki za wenzake na kuheshimu maoni ya wengine.

(14) Kushirikiana na serikali ya nchi na kujitolea muhanga nafsi yake pale adui wa nje anapoivamia au kuihujumu nchi yetu kwa uhasama, ubabe na matumizi ya maguvu yanayoweza kuleta madhara kwa wananchi na nchi yao.

(15) Kupambana na serikali yoyote ya nchi kwa hoja na njia za kidemokrasia na ikiwa serikali hiyo imeanza au inaelekea kuanzisha mfumo wa utawala wa mabavu na udikteta kwa raia wake.

(16) Kukilinda Chama kutokana na maadui wa ndani au wa nje wanaokusudia kukihujumu, kukiua, kukigawa au kukidhoofisha.

SURA YA TATU

MUUNDO, NGAZI ZA VIKAO NA VIONGOZI WA CHAMA

SEHEMU YA KWANZA

MUUNDO WA CHAMA

Muundo wa Chama

13. (1) Kwa madhumuni ya kuwa karibu na watu na bila ya kuwa na muundo mzito, na kwa nia ya kushika hatamu za dola, Chama kitakuwa na muundo wa ngazi tano kama ifuatavyo:-

a) Ngazi ya Tawi kwa Tanzania nzima
b) Ngazi ya Kata kwa Tanzania Bara
c) Ngazi ya Jimbo kwa Tanzania nzima
d) Ngazi ya Wilaya kwa Tanzania nzima
e) Ngazi ya Taifa kwa Tanzania nzima.

(2) Vikao vya ngazi ya Chama husika vitakuwa kama itavyoelezwa katika ngazi yenyewe

(3) Kwa ngazi ya Taifa kutakuwa na vikao vya maamuzi kwa mpangilio wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Kamati ya Utendaji ya Taifa, na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa.

Maamuzi ya Chama

14. (1) Mapendekezo yoyote ya kuimarisha au kuendeleza Chama yanaweza kutoka ngazi ya chini kwenda ngazi ya juu kwa kufanyiwa kazi na maamuzi yatatoka ngazi ya juu kwenda ngazi ya chini kwa utekelezaji.

(2) Katika ngazi moja yeyote ile, mapendekezo yatatoka katika kikao cha chini kwenda kikao cha juu kwa kufanyiwa kazi na maamuzi yatatoka kikao cha juu kwenda kikao cha chini kwa utekelezaji.

(3) Bila ya kuathiri kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, mapendekezo yoyote ya kuimarisha Chama yanaweza pia yakatoka katika ngazi moja na kufanyiwa kazi na ngazi hiyo hiyo na kwamba inaweza pia kutoa uamuzi wake ambao unaweza kusahihishwa au kubatilishwa na ngazi yoyote iliyopo juu yake.

(4) Bila ya kuathiri kijifungu cha (2) cha kifungu hiki, mapendekezo yote ya kuimarisha chama yanaweza pia yakatoka katika kikao kimoja na kufanyiwa kazi na kikao hicho na kwamba kinaweza pia kutoa uamuzi wake ambao unaweza kusahihishwa au kubatilishwa na kikao chochote kilichopo juu yake

SEHEMU YA PILI

NGAZI YA TAWI

Tawi

15. (1) Tawi la Chama linajumuisha eneo la kijiji au vijiji, mtaa au mitaa ambayo imeelezwa hivyo kwa mujibu wa sheria, na kulingana na hali halisi ya pahala hapo. Isipokuwa kwamba katika kijiji au mtaa mmoja kunaweza kuwa za zaidi ya tawi moja la Chama.

(2) Tawi linaweza kufunguliwa pahala popote pale ikiwa patakuwa na wanachama wasiopungua hamsini (50) na kwamba pale ambapo tawi moja limezidi wanachama mia nne (400) basi tawi hilo kwa kukubaliana na uongozi wa Kata/Jimbo na Wilaya pale inapoonekana inafaa, linaweza likaanzishwa tawi jingine.

(3) Ofisi ya tawi ni chumba, nyumba, banda au nafasi iliyotengwa maalum kwa shughuli za Chama za kila siku. Eneo hilo liwe na bendera ya Chama na alama nyingine zilizo wazi zinazoonekana na kila mwanachama pamoja na wananchi wengine wote.

(4) Bendera na alama nyingine ya Chama inaweza kuwekwa mahala pengine popote pale penye mwanachama au wanachama.

Muundo wa Tawi

16. (1) Tawi litakuwa na vikao vifuatavyo vya Chama:
a) Mkutano Mkuu
b) Kamati ya Utendaji
c) Kamati ya Ulinzi na Usalama

Mkutano Mkuu wa Tawi

17. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Tawi ambao utakutana katika vikao vya kawaida mara moja baada ya kila miezi mitatu. Ikitokea dharura Kamati ya Utendaji ya Tawi inaweza kuitisha Mkutano Mkuu wa Tawi wakati wowote ule.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi watakuwa ni Wanachama wote wa Chama waliopo katika tawi hilo.

Wajibu wa Mkutano Mkuu

18. (1) Mkutano Mkuu wa Tawi ndicho kikao kikuu kupita vyote katika Tawi na wajibu wake utakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya:-

(i) Utendaji wa shughuli za Chama katika eneo la Tawi.
(ii) Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha ya kila miezi minne.
(iii) Mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya Tawi ya kila mwaka.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya kuendeleza na kuimarisha Chama katika eneo la Tawi.
(v) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi katika eneo la Tawi.
(vi) Kujenga na kuendeleza udugu wa dhati miongoni mwa wanachama wa Chama na wananchi wengine katika eneo la Tawi.
(vii) Kuwa na uamuzi na kauli ya mwisho katika mambo yote ya Chama katika eneo la Tawi.
(viii) Kutoa pongezi, sifa, zawadi au motisha kwa mwanachama yeyote wa Tawi hilo pale inapofaa kufanya hivyo.
(ix) Kumchukulia hatua za nidhamu mwanachama au kiongozi yeyote wa Tawi hilo, ikiwa ni pamoja na kumpa onyo, karipio, karipio kali, kumsimamisha uanachama au uongozi wa Chama kwa muda, na hata kumuachisha au kumfukuza uanachama wa Chama.

(2) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama Mkutano Mkuu wa tawi utawachagua viongozi wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa tawi

(ii) Katibu wa tawi

(iii) Mweka hazina wa tawi

(iv) Wajumbe watano (5), angalau wawili (2) wakiwa ni wanawake kutoka miongoni mwa wanachama wa Tawi hilo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata kwa upande wa Tanzania Bara na wajumbe kumi (10), angalau watatu(3) wakiwa ni wanawake, kutoka miongoni mwa wanachama wa Tawi hilo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa upande wa Zanzibar.

(v) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (3) wakiwa ni wanawake kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya tawi hilo.

(3) Mkutano Mkuu wa Tawi utasimamia masuala yote ya Haki za Binadamu na Haki za Watu katika eneo la Tawi, na inapobidi, kuchukua hatua zinazofaa katika kulinda na kutetea haki hizo kwa mwananchi wa eneo la Tawi hilo ambaye anastahiki ulinzi na utetezi wa haki zake hizo.

(4) Mkutano Mkuu wa Tawi utahakikisha utekelezaji mzuri wa maamuzi yake na maamuzi ya vikao vya ngazi za juu yake vya Chama.

(5) Mkutano Mkuu wa Tawi utaongozwa na Mwenyekiti wa Tawi hilo, na iwapo Mwenyekiti wa Tawi hataweza kuhudhuria kikao chochote cha Mkutano Mkuu wa Tawi, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi atakayechaguliwa na kikao chenyewe, isipokuwa Katibu wa Tawi na Mweka Hazina wa Tawi. Mjumbe huyo aliyechaguliwa atakuwa Mwenyekiti wa muda na ataongoza kikao hicho tu.

Kamati ya Utendaji ya Tawi

19. (1) Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Tawi itakayokutana kwa vikao vya kawaida angalau mara moja kila baada ya mwezi mmoja isipokuwa pale itakapotokea haja ya dharura na ulazima ambapo inaweza kukutana wakati wowote.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi watakuwa kama ifuatavyo:-

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Tawi

a) Mwenyekiti wa Tawi
b) Katibu wa Tawi
c) Mweka hazina wa Tawi
d) Wajumbe wengine kumi (10), angalau watatu (3) wakiwa ni wanawake waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi.
e) Diwani wa Chama hiki anayeishi katika eneo la Tawi hilo.
f) Mbunge/Mwakilishi na kiongozi yeyote wa Kitaifa wa Chama hiki anayeishi katika eneo la Tawi hilo.
g) Wenyeviti wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji wa Chama hiki wanaoishi katika eneo la tawi hilo.

Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Tawi

20. (1) Kamati ya Utendaji ya Tawi itakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

a) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Mkutano Mkuu wa Tawi na vikao vingine vya ngazi za juu.
b) Kuwahamasisha wananchi wajiunge na Chama na kutetea na kueneza itikadi ya Chama na sera za Chama katika eneo lake.
c) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Tawi.
d) Kutekeleza kazi za kila siku za Chama katika eneo la Tawi.
e) Kutunza, kuhifadhi na kulinda mali, vyombo, nyaraka na mihuri ya Chama iliyomo katika Tawi.
f) Kusimamia mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa wanachama wa tawi.
g) Kuhakikisha kwamba haki za binadamu za kila mtu katika Tawi zinaheshimiwa na kuenziwa.
h) Kujenga uhusiano mzuri na vikundi mbali mbali vya wananchi katika eneo lake na kutoa miongozo ya kisiasa kwa wanachama katika Tawi.

i) Kushirikiana na vyombo vya dola vilivyomo katika eneo la Tawi hilo katika kulinda na kuendeleza amani na utulivu, kujenga, kuendeleza na kusimamia huduma za kiuchumi na za kijamii katika eneo lake.

j) Kulinda na kusimamia uhai wa Chama na wa wanachama pamoja na utekelezaji wa itikadi, sera na programu za chama katika eneo la Tawi.

k) Kusimamia miradi ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, pamoja na sherehe na tafrija za Chama katika eneo la Tawi.

l) Kushirikiana na vyombo vingine vya jamii katika kutoa huduma muhimu kwa wazee wasiojiweza, watoto wanaohitaji kusaidiwa, na wananchi wengine waliofikwa na maafa katika eneo la Tawi.

(2) Wakati wa uchaguzi wa nchi wenye kushirikisha vyama vingine vya siasa, Kamati ya Utendaji ya Tawi itafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kuhakikisha ushindi wa wagombea wa Chama katika uchaguzi wowote utakaohusisha vyama vingine vya siasa kwa kupiga kampeni halali kwa mujibu wa sheria za nchi.

(b) Kushirikiana na viongozi na maofisa wa ngazi za juu za Chama katika kuteua wanachama wanaofaa kuwa wasimamizi na au mawakala wa wagombea uchaguzi wa Chama, pamoja na msimamo wa Chama katika kura ya maoni, katika vituo vya kuandikishwa wapiga kura na vya kupigia kura ili kuhakikisha kwamba kura za mgombea wa Chama, au msimamo wa Chama katika Kura ya maoni hazichakachuliwi, hazivurugwi na wala haziibiwi, na pia kuweza kufichua njia zozote za udanganyifu.

21. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi itayokutana angalau mara moja kwa kila wiki

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi

a) Kamati ya ulinizi na usalama itaongozwa na Mwenyekiti wa Tawi na itakuwa na wajumbe wengine wafuatao:-

(i) Katibu wa Tawi

(ii) Kamanda wa Blue Guards wa Tawi

(iii) Wanachama wawili wa Tawi hilo, mmoja mwanamke na mwengine mwanamme kutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Tawi baada ya kushauriana na Katibu wa Tawi.

22. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi ni kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama katika eneo zima la Tawi.

(2) Kukikinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kikodhoofisha katika eneo zima la Tawi.

(3) Kuhakikisha ulinzi wa Viongozi Wakuu wa Chama wa Tawi, mali za Chama, majengo ya Chama na shughuli nyingine zote za Chama katika Tawi.

(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama katika Tawi.

23. Kutakuwa na Viongozi Wakuu wafuatao wa Chama katika ngazi ya Tawi:-

Viongozi Wakuu wa Tawi

a) Mwenyekiti

(b) Katibu

(c) Mweka hazina

24. Mwenyekiti wa Tawi atakuwa na majukumu yafuatayo:

Kazi za Mwenyekiti wa Tawi

(1) Ndiye atakayekuwa kiongozi mkuu wa shughuli za Chama na msemaji mkuu wa Chama katika eneo la Tawi.

(2) Ataongoza vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Tawi, Kamati ya Utendaji ya Tawi na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Tawi.

(3) Atakuwa na kura ya uamuzi endapo katika mkutano wa kikao anachokiongoza kura zitafungana.

(4) Atatoa kadi kwa wanachama wapya waliokubalika kujiunga na Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

25. Katibu wa Tawi atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Katibu wa Tawi

(1) Atakuwa mtendaji mkuu wa Chama na mwajibikaji mkuu wa shughuli zote za utendaji za Chama katika eneo la Tawi.

(2) Atafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Mwenyekiti wa Tawi na Mweka hazina wa Tawi.

(3) Atakuwa dhamana wa ofisi ya Tawi.

(4) Atahakikisha kwamba nyaraka za Chama katika Tawi zinatunzwa na kuhifadhiwa.

(5) Atasimamia kuandikwa na kuhifadhiwa kumbukumbu za vikao vyote vya Chama tawini.

(6) Atakuwa mwajibikaji mkuu wa mambo yote ya fedha na mali za Chama katika Tawi lake.

(7) Atatunza daftari la wanachama wote katika Tawi hilo, na

(8) Atafanya kazi nyingine zote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Tawi, Kamati ya Utendaji ya Tawi, vikao vya juu, Mwenyekiti wa tawi, na katibu wa Kata/Jimbo.

26. Mweka Hazina wa tawi atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mweka Hazina wa Tawi

(1) Kutunza mali na fedha za Chama na madaftari ya mahesabu yote ya fedha na ya mali za Chama na kuyaweka tayari kwa ukaguzi wa ndani ya Chama wakati wote.

(2) Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Chama katika tawi.

(3) Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya tawi na ngazi za juu.

(4) Kubuni miradi ya uchumi katika tawi na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya tawi na ngazi za juu.

(5) Kukusanya mapato ya Chama katika tawi na kufanya malipo yote yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa kanuni za fedha na taratibu nyengine za Chama kama zilivyowekwa katika Kanuni zitakazotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuidhinishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

27. (1) Kiongozi mkuu yeyote wa tawi anaweza kusimamishwa uongozi na Mkutano Mkuu wa Tawi na kisha kufikisha taarifa ya sababu zake kwa Kamati ya Utendaji ya Kata/Jimbo nayo kwa kutoa maoni na mapendekezo yake.

Kusimamishwa/ kufukuzwa kwa Viongozi Wakuu wa Tawi

(2) Kamati ya Utendaji ya wilaya ndiyo yenye mamlaka ya kumchukulia hatua za nidhamu, zikiwemo kumpa onyo, karipio, karipio kali na hata kumuachisha au kumfukuza uongozi kiongozi mkuu wa tawi endapo tuhuma dhidi yake zitathibitika.

(3) Endapo Kiongozi Mkuu wa Tawi ataachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki, basi Kiongozi aliyeathirika atakuwa na haki ya kukata Rufaa kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa, na ikiwa hakuridhika, ataweza kukata rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambalo uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Endapo Kiongozi Mkuu wa Tawi atasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii mwanachama wa kukaimu nafasi hiyo ya uongozi atachaguliwa kwa mujibu wa masharti ya vifungu vya 104 (1) na (3) vya Katiba hii.

28. (1) Kutakuwa na Mratibu wa Chama atakayewawakilisha wanachama katika vikundi vifuatavyo:-

Mratibu wa Chama

(a) Katika kila nyumba ishirini katika mtaa, kijiji/kitongoji.

(b) Kwenye mkusanyiko wa kawaida wa wananchi kama masoko, mabaraza, vituo vya mabasi na, taxi na kadhalika, au

(c) Pahala pengine popote ambapo Kamati ya Utendaji ya Tawi itaamua

(2) Mratibu wa Chama atateuliwa na Kamati ya Utendaji ya Tawi baada ya kushauriana na wanachama wa eneo linalohusika.

29. Kazi za Mratibu wa Chama zitakuwa ni

(1) Kupokea maagizo kutoka tawini na kuyafikisha kwa wanachama wa eneo lake.

Kazi za Mratibu wa Chama

(a) Kusimamia uhai wa Chama katika eneo lake.
(b) Kutayarisha na kuhifadhi daftari la wanachama katika eneo lake.
(c) Kuhamasisha wanachama kushiriki katika shughuli za Chama au Jumuiya za Chama katika eneo lake.
(d) Kubuni vivutio vitakavyowavutia wananchi wengi kujiunga na Chama ikiwa ni pamoja vikundi vitavyojishughulisha na miradi ya kiuchumi, michezo mbali mbali kama keram, karata, na kadhalika.
(e) Kuwashawishi wananchi katika eneo lake kuwapigia kura wagombea wa Chama katika uchaguzi wa kiserikali unaohusisha vyama vyengine vya siasa au msimamo wa Chama katika kura ya maoni.
(f) Kufanya kazi nyengine yoyote atakayopewa na uongozi wa tawi au vikao vya juu.

SEHEMU YA TATU

NGAZI YA KATA

30. (1) Ngazi hii itatumika kwa Tanzania Bara tu, na ni eneo la shughuli za Serikali ambalo limeelezewa katika sheria za Tanzania Bara zinazohusika.

Kata na Muundo wake

(2) Kata itakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu wa Kata.
(b) Kamati ya Utendaji ya Kata.
(c) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata.

31. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Kata ambao utakutana kwa vikao vya kawaida mara moja kwa kila miezi sita, isipokuwa kwa pale itapotokea dharura, Mkutano Mkuu wa Kata unaweza kuitishwa wakati wowote ule na Kamati ya Utendaji ya Kata.

Mkutano Mkuu wa Kata

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata watakuwa:-

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata

(a) Mwenyekiti wa Kata,

(b) Katibu wa Kata,

(c) Mweka hazina wa Kata,

(d) Mwenyekiti na Katibu wa kila Tawi lililomo ndani ya Kata hiyo,

(e) Wajumbe watano (5), angalau wawili wakiwa ni wanawake waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Tawi lililomo katika kata hiyo.

(f) Mbunge atokanaye na Chama hiki na/au kiongozi yeyote wa Kitaifa wanao/anayeishi katika Kata hiyo.

(g) Madiwani wanaowakilisha Kata hio au wanaoishi katika Kata hiyo watokanao na Chama hiki.

(h) Wenyeviti wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji vya Kata hiyo watokanao na Chama hiki.

32. (1) Mkutano Mkuu wa Kata ndio kikao kikuu kupita vyote katika eneo la Kata na wajibu wake utakuwa kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Kata

a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya:-

(i) Taarifa za utendaji wa shughuli za Chama katika eneo la Kata, zikijumuisha taarifa za matawi yote yaliyomo katika Kata.

(ii) Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama katika Kata kwa kila miezi mitatu.

(iii) Mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya fedha za Chama ya kila mwaka ya Kata.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya kuendeleza na kuimarisha Chama katika eneo la Kata.

(v) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi katika eneo la Kata.

b) Kujenga na kuendeleza udugu wa dhati miongoni mwa Wanachama wa Chama na wananchi wengine katika eneo la Kata.

c) Kuwa na uamuzi na kauli ya mwisho katika mambo yote ya Chama katika eneo la Kata.

d) Kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya kiongozi yeyote wa Kata na wa ngazi ya chini pamoja na kusikiliza Rufaa kutoka viongozi na wanachama waliochukuliwa hatua za nidhamu na vikao vya chini.

(2) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama Mkutano Mkuu wa Kata utawachagua viongozi wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Kata

(ii) Katibu wa kata

(iii) Mweka hazina wa Kata

(iv) Wajumbe kumi na watano (15), angalau watano (5) wakiwa ni wanawake kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata kutoka miongoni mwao.

(v) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (3) wakiwa ni wanawake kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya kutoka miongoni mwao.

(vi) Vijana wawili (2), mmoja mwanamume na mmoja mwanamke kutokana na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(vii) Wanawake wawili (2) kutokana na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(viii) Wazee wane (4), wawili (2) wanawake na wawili (2) wanaume kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(3) Mkutano Mkuu wa Kata pia utakuwa na wajibu wa:-

(a) Kusimamia masuala yote ya haki za binadamu na haki za watu katika eneo la Kata hiyo, na ikibidi kuchukua hatua zinazofaa katika kulinda na kutetea haki hizo kwa mwananchi yeyote anayeishi katika eneo la Kata hiyo ambaye atastahili ulinzi na utetezi wa haki zake hizo.

(b) Kuhakikisha utekelezaji mzuri wa maamuzi yake na maamuzi ya vikao vya ngazi za juu yake vya Chama.

(4) Mkutano Mkuu wa Kata utaongozwa na Mwenyekiti wa Kata hiyo, na Mwenyekiti asipoweza kuhudhuria kikao chochote cha Mkutano Mkuu wa Kata, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata aliyechaguliwa na kikao chenyewe isipokuwa Katibu wa Kata na Mweka Hazina wa Kata. Mjumbe huyo atakuwa Mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

Kamati ya Utendaji ya Kata

33. Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Kata itakayokutana kwa vikao vya kawaida angalau mara moja kwa kila mwezi isipokuwa pale itakapotokea haja ya dharura na ya ulazima ambapo inaweza kukutana wakati wowote ikiwa Mwenyekiti wa Kata, baada ya kushauriana na Katibu wa Kata ataamuru hivyo.

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata

34. (1) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Kata watakuwa wafuatao
a) Mwenyekiti wa Kata.
b) Katibu wa Kata.
c) Mweka Hazina wa Kata.
d) Wajumbe wengine kumi na watano (15), angalau watano (5) wakiwa ni wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata kutokana miongoni mwao.

e) Diwani wa Chama hiki anayewakilisha Kata hiyo au anayeishi katika Kata hiyo.
f) Mbunge wa Chama hiki au kiongozi yeyote wa Kitaifa wa Chama anayeishi katika Kata hiyo.

35. (1) Kamati ya Utendaji ya Kata itakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Kata

a) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Mkutano Mkuu wa Kata na vikao vya ngazi za juu.
b) Kusimamia uenezi wa itikadi, sera na programu za Chama katika Kata.
c) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Kata.
d) Kusimamia mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa wanachama na viongozi wa Chama wa Kata.
e) Kuhakikisha kwamba haki za binadamu za kila mtu katika eneo la Kata zinaheshimiwa na kuenziwa.
f) Kusimamia vikundi mbalimbali vya wanachama hasa katika kutekeleza miradi ya kiuchumi na kuendeleza utamaduni na michezo katika eneo la Kata.
g) Kushirikiana na vyombo vya dola vilivyomo katika eneo la Kata hiyo katika kulinda na kuendeleza amani na utulivu, kujenga, kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi na za kijamii.
h) Kulinda na kusimamia uhai wa Chama, wanachama na utekelezaji wa itikadi, sera na program za Chama katika eneo la Kata.
i) Kusimamia miradi ya uchumi, kijamii, kimaendeleo na kiutamaduni, pamoja na sherehe na tafrija za Chama katika eneo la Kata.
j) Kushirikiana na vyombo vingine vya jamii katika usimamizi wa utoaji wa huduma muhimu kwa wazee wasiojiweza, watoto wanaohitaji kusaidiwa na wananchi wengine waliofikwa na maafa katika eneo la Kata.

(2) Wakati wa uchaguzi wa nchi unaohusisha vyama vingine vya siasa Kamati ya Utendaji ya kata itafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kuandaa kampeni katika eneo la Kata kwa kushirikiana na viongozi na maofisa wa ngazi za juu za Chama na Kamati za Utendaji za matawi yaliyomo katika Kata hiyo ili kuhakikisha mgombea wa Chama anapata kura nyingi katika eneo la kata hiyo na kushinda.

(b) Kwa kushirikiana na viongozi na maofisa wa ngazi za juu za Chama, kutoa maelekezo kwa Kamati za Utendaji za matawi yaliyomo katika Kata hiyo kuhusu uteuzi wa wanachama wanaofaa kuwa wasimamizi na, au mawakala wa wagombea wa Chama, pamoja na msimamo wa Chama katika kura ya maoni, katika vituo vya kuandikishwa wapiga kura na vya kupigia kura na kusimamia uteuzi huo kwa karibu.

(3) Kamati ya Utendaji ya Kata itaongozwa na Mwenyekiti wa Kata hiyo, na Mwenyekiti huyo asipoweza kuhudhuria kikao chochote cha Kamati hiyo, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe mwingine yeyote wa kikao hicho aliyechaguliwa na kikao chenyewe isipokuwa Katibu wa Kata na Mweka Hazina wa Kata. Mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

36. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata itayokutana angalau mara moja kwa kila wiki.

Kamati ya na Ulinzi na Usalama ya Kata

(2) Kamati ya Ulinzi na Usalama itaongozwa na Mwenyekiti wa Kata na itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i) Katibu wa Kata
(ii) Kamanda wa Blue Guards wa Kata
(ii) Wanachama wawili wa Kata hiyo mmoja mwanamke na mmoja wanamme kutokana na wajumbe wa Makutano Mkuu wa Kata watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Kata hiyo baada ya kushauriana na Katibu wa Kata.

37. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata ni kama ifuatavyo:-

Wajibu wa wa Kamati ya Ulinzi na Usalama

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama katika eneo zima la Kata.

(2) Kukinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kikodhoofisha Chama katika Kata.

(3) Kuhakikisha ulinzi wa Viongozi Wakuu wa Chama wa Kata, mali za Chama, majengo ya Chama na shughuli nyingine zote za Chama katika Kata.

(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama katika Kata.

(5) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata inaweza, kwa maslahi ya Chama kutoa maelekezo ya kiulinzi au maelekezo mengine yoyote inayohisi yanafaa kwa Kamati za Ulinzi za ngazi ya Tawi na Kamati hizo zitawajibika kutekeleza maagizo hayo kwa utaratibu uliotolewa na baadae kutoa taarifa ya utendaji kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Kata.

38. Kutakuwa na viongozi wakuu wafuatao wa Chama katika ngazi ya Kata.

Viongozi Wakuu wa Kata

(1) Mwenyekiti wa Kata.

(2) Katibu wa Kata.

(3) Mweka Hazina wa Kata.

39. Mwenyekiti wa Kata atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mwenyekiti wa Kata

(1) Ndiye atakayekuwa Kiongozi Mkuu wa shughuli za Chama katika eneo la Kata na atakuwa msemaji mkuu wa Chama katika eneo la Kata.

(2) Ataongoza vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Kata na Kamati ya Utendaji ya Kata.

(3) Atakuwa na kura ya uamuzi endapo katika mkutano wa kikao anachokiongoza kura za wajumbe zitafungana.

(4) Atakiwakilisha Chama katika shughuli za kiserikali na kijamii katika eneo la Kata.

40. Katibu wa Kata atakuwa na kazi zifuatazo:-

Kazi za Katibu wa Kata

(1) Atakuwa mtendaji mkuu wa Chama na mwajibikaji mkuu wa shughuli za utendaji zote za Chama katika eneo la Kata yake.

(2) Atafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Mwenyekiti wa Kata na Mweka hazina wa Kata.

(3) Atakuwa dhamana wa ofisi ya Chama katika Kata hiyo

(4) Atahakikisha kwamba nyaraka za Chama katika Kata zinatunzwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

(5) Atahakikisha kuwepo na kuhifadhiwa kwa kumbukumbu za vikao vyote vya Chama katika Kata.

(6) Atakuwa mwajibikaji mkuu wa mambo yote ya fedha na mali za Chama katika Kata.

(7) Atatayarisha na kutunza madaftari ya viongozi na wanachama wa Chama wa matawi yote yaliyomo katika Kata yake.

(8) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Kata, Kamati ya Utendaji ya Kata, Mwenyekiti wa Kata na Katibu wa wilaya.

41. Mweka Hazina wa kata atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mweka Hazina wa Kata

(1) Kutunza mali na fedha za Chama na madaftari ya mahesabu yote ya fedha katika Kata na kuyaweka tayari kwa ajili ya ukaguzi wa ndani ya Chama wakati wote.

(2) Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Chama katika Kata.

(3) Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Kata na ngazi za juu.

(4) Kubuni miradi ya uchumi katika Kata na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya Kata na ngazi za juu.

(5) Kukusanya mapato ya Chama na kufanya malipo yote katika Kata yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha na taratibu nyingine za Chama kama zitakazotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuidhinishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(6) Kufuatilia ukusanyaji wa mapato yote katika matawi yaliyomo katika Kata yake.

Kusimamishwa/ Kufukuzwa Uongozi Viongozi Wakuu wa Kata

42. (1) Kiongozi Mkuu wa Kata anaweza kusimamishwa uongozi na Mkutano Mkuu wa Kata baada ya kupokea mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Kata.

(2) Kamati ya Utendaji ya wilaya ndiyo yenye mamlaka ya kumchukulia hatua nyengine za nidhamu Kiongozi Mkuu wa Kata, zikiwemo onyo, karipio, karipio kali na hata kumuachisha au kumfukuza uongozi Kiongozi Mkuu yeyote wa Kata baada ya kupokea mapendekezo ya Mkutano Mkuu wa Kata na endapo tuhuma dhidi yake zitathibitika.

(3) Endapo Kiongozi Mkuu wa Kata ataachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya kifungu hiki, basi Kiongozi Mkuu huyo atakuwa na haki ya kukata Rufaa kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa, na asiporidhika, ataweza kukata rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambalo uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Endapo Kiongozi Mkuu wa Kata atasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya Kifungu hiki mwanachama wa kukaimu nafasi hiyo ya uongozi atachaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 104(1) na(3) vya Katiba hii.

SEHEMU YA NNE

NGAZI YA JIMBO

Jimbo na Muundo wake

43. Ngazi hii ya jimbo itatumika kwa Tanzania nzima, na Jimbo ni eneo la uchaguzi kama lilivyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar au Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumchagua Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Mbunge.

Jimbo kwa Zanzibar

44. (1) Muundo na Shughuli za Ngazi ya Jimbo Kwa upande wa Zanzibar utakuwa kama vifuatavyo.:-

(2) Jimbo litakuwa na vikao vifuatavyo

(i) Mkutano Mkuu wa Jimbo
(ii) Kamati ya Utendaji ya Jimbo
(ii) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo

Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa Zanzibar

45. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo ambao utakutana katika vikao vya kawaida kila baada ya miezi sita, isipokuwa kwamba ikitokea dharura muhimu, Kamati ya Utendaji ya Jimbo inaweza kuitisha kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa Jimbo wakati wowote ule.

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo watakuwa wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Jimbo.

(b) Katibu wa Jimbo.

(c) Mweka Hazina wa Jimbo.

(d) Mwenyekiti na Katibu wa kila Tawi lililomo katika Jimbo hilo.

(e) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (03) wakiwa ni wanawake waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Tawi lililomo katika Jimbo hilo.

(f) Mbunge/Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo hilo na yule anayeishi ndani ya Jimbo hilo watokanao na Chama, na kiongozi yeyote wa Chama wa Kitaifa aishiye katika jimbo hilo.

(g) Madiwani waliomo ndani ya Jimbo hilo watokanao na Chama.

(h) Wenyeviti wa halmashauri za wilaya/mji watokanao na Chama wanaoishi katika jimbo hilo.

46. (1) Mkutano Mkuu wa Jimbo ndicho kikao kikuu kupita vyote katika eneo la Jimbo na wajibu wake utakuwa kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Jimbo kwa Zanzibar

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya:-

(i) Taarifa za utendaji wa shughuli za Chama katika eneo la Jimbo.

(ii) Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama katika Jimbo za kila miezi sita.

(iii) Mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya fedha za Chama ya kila mwaka katika jimbo.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya kuendeleza na kuimarisha Chama katika eneo la jimbo.

(v) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo kiuchumi katika eneo la Jimbo.

(b) Kujenga na kuendeleza udugu wa dhati miongoni mwa wanachama na wananchi wengine katika eneo la Jimbo.

(c) Kuwa na uamuzi na kauli ya mwisho katika mambo yote ya Chama katika eneo la Jimbo.

(d) Kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya kiongozi yoyote wa Jimbo na wa ngazi ya chini, pamoja na kusikiliza Rufaa kutoka viongozi na wanachama waliochukuliwa hatua za kinidhamu na vikao vya chini.

(e) Kupokea, kuyajadili na kuyatolea uamuzi maoni ya wananchi katika Jimbo, kuhusu mambo ya siasa, maendeleo ya uchumi na jamii na kero za wananchi wa Jimbo hilo ili kuwashawishi wananchi waunge mkono Chama.

(2) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama Mkutano Mkuu wa Jimbo utawachagua viongozi wafuatao:

(i) Mwenyekiti wa Jimbo.

(ii) Katibu wa Jimbo

(iii) Mweka Hazina wa Jimbo

(iv) Wajumbe kumi na watano (15), angalau watano (05) wakiwa niwanawake, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya, kutoka miongoni mwao.

(v) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (03) wakiwa ni wanawake, kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo, kutoka miongoni mwao.

(vi) Vijana wawili (02), mmoja mwanamme na mmoja mwanamke, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya, kutoka miongoni mwao.

(vii) Wanawake wawili (02) kutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(viii) Wazee wane (04), wawili (02) wanawake na wawili (02) wanaume kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo kuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(3) Mkutano Mkuu wa Jimbo pia utakuwa na wajibu ufuatao:

(a) Kufuatilia masuala yote ya haki za binadamu na haki za watu katika eneo la Jimbo.

(b) Kuhakikisha utekelezaji mzuri wa maamuzi yake na maamuzi ya vikao vya ngazi za juu vya Chama.

(4) Mkutano Mkuu wa Jimbo utaongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo na asipoweza kuhudhuria kikao chochote cha Mkutano Mkuu wa Jimbo, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe mwingine yeyote wa kikao hicho aliyechaguliwa na kikao chenyewe isipokuwa Katibu wa Jimbo na Mweka hazina wa Jimbo. Mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

Kamati ya Utendaji ya Jimbo

47. Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Jimbo itakayokutana kwa vikao vya kawaida angalau mara moja kwa kila mwezi isipokuwa pale itapotokea haja ya dharura na ya ulazima ambapo inaweza kukutana wakati wowote ule kama itavyoamuliwa na Mwenyekiti wa Jimbo baada ya kushauriana na Katibu wa Jimbo.

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo

48. Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo watakuwa wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Jimbo

(b) Katibu wa Jimbo

(c) Mweka Hazina wa Jimbo

(d) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (3) wakiwa wanawake waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Jimbo.

(e) Madiwani waliomo ndani ya Jimbo hilo.

(f) Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo hilo na yule anayeishi katika jimbo hilo watokanao na Chama na kiongozi yeyote wa Chama wa Kitaifa aishiye ndani ya Jimbo hilo.

49. (1) Kamati ya Utendaji ya Jimbo itakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Jimbo

(a) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Jimbo na ya vikao vya ngazi za juu.

(b) Kusimamia uenezi wa itikadi, sera na programu za Chama katika Jimbo.

(c) Kuunda mikakati na mbinu za kuwashawishi wananchi waunge mkono sera, programu na misimamo ya Chama katika Jimbo ili Chama kukubalike katika Jimbo.

(d) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Jimbo.

(e) Kusimamia mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa wanachama na viongozi wa Chama katika Jimbo.

(f) Kuhakikisha kwamba kila mwananchi anatendewa haki na kwa yule anayeonewa basi Kamati ya Utendaji ya Jimbo imsaidie kwa kufuata sheria na taratibu za nchi.

(g) Kuhamasisha uundwaji wa vikundi mbali mbali vya wanachama na wananchi wengine katika Jimbo na kuvisimamia vikundi hivyo katika kutekeleza miradi ya uchumi, pamoja na kuendeleza utamaduni na michezo.

(h) Kushirikiana na vyombo vya dola vilivyomo katika Jimbo katika kulinda na kuendeleza amani na utulivu, kujenga, kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi na za kijamii katika Jimbo.

(i) Kusimamia miradi ya uchumi, sherehe na tafrija za Chama katika Jimbo.

(j) Kushirikiana na vyombo vyengine vya jamii katika usimamizi wa utoaji huduma

muhimu kwa wazee wasiojiweza, watoto wanaohitaji kusaidiwa, na wananchi wengine waliofikwa na maafa katika Jimbo.

(k) Kushirikiana na Mbunge na Mwakilishi wa Jimbo na yule anayeishi katika jimbo hilo watokanao na Chama katika kushughulikia kero, matatizo sugu na matatizo mengine ya wananchi katika jimbo hilo.

(2) Wakati wa uchaguzi wa nchi unaohusisha vyama vingine vya siasa, Kamati ya Utendaji ya Jimbo itafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kuandaa kampeni katika Jimbo kwa kushirikiana na Viongozi na maofisa wa ngazi za juu za Chama, Kamati za Utendaji za matawi, na Kamati ya Utendaji ya Wilaya ili kuhakikisha kwamba mgombea wa Chama anashinda.

(b) Kufuatilia kwa karibu uteuzi wa wanachama wanaoteuliwa kuwa wasimamizi na, au mawakala wa wagombea wa Chama na msimamo wa Chama katika kura ya maoni, katika vituo vya kuandikishwa wapiga kura na vya kupigia kura na kutoa maelekezo kwa Kamati za Utendaji za matawi kuhusu jambo hilo.

(3) Kamati ya Utendaji ya Jimbo itaongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo, na asipoweza kuhudhuria kikao chochote cha Kamati hiyo, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe mwingine yeyote wa kikao hicho; isipokuwa Katibu wa Jimbo na Mweka Hazina wa Jimbo, aliyechaguliwa na kikao chenyewe. Mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

50. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo itayokutana angalau mara moja kwa kila baada ya wiki mbili.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo kwa Zanzibar

(2) Kamati ya Ulinizi na Usalama ya Jimbo itaongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo na itakuwa na wajumbe wengine wafuatao :

(i) Katibu wa Jimbo.
(ii) Kamanda wa Blue Guards wa Jimbo.
(iii) Wanachama wawili wa Jimbo hilo mmoja mwanamke na mwengine mwanamme kutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Jimbo baada ya kushauriana na Katibu wa Jimbo.
(iv) Mbunge na Mwakilishi wanaowakilisha Jimbo hilo au wanaoishi katika Jimbo hilo.

51. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo ni kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama katika eneo zima la Jimbo.

(2) Kukikinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kikodhoofisha katika Jimbo.

(3) Kuhakikisha ulinzi wa Viongozi Wakuu wa Chama wa Jimbo, mali za Chama, majengo ya Chama na shughuli nyingine zote za Chama katika Jimbo.

(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama katika Jimbo.

(5) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo inaweza, kwa maslahi ya Chama, kutoa maelekezo ya kiulinzi au maelekezo mengine yoyote inayohisi yanafaa kwa Kamati za Ulinzi na Usalama za matawi, na Kamati hizo zitawajibika kutekeleza maagizo hayo kwa utaratibu uliotolewa na baadae kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo.

52. Kutakuwa na Viongozi Wakuu wafuatao katika Jimbo:-

Viongozi Wakuu wa Jimbo

(1) Mwenyekiti wa Jimbo

(2) Katibu wa Jimbo

(3) Mweka Hazina wa Jimbo

53. Mwenyekiti wa Jimbo atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mwenyekiti wa Jimbo

(1) Ndiye atakayekuwa Kiongozi Mkuu wa shughuli zote za Chama katika Jimbo, na atakuwa msemaji mkuu wa Chama katika Jimbo.

(2) Ataongoza vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Jimbo, Kamati ya Utendaji ya Jimbo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo.

(3) Atakuwa na kura ya uamuzi endapo katika kikao anachokiongoza kura za wajumbe zitafungana.

(4) Atakiwakilisha Chama katika shughuli za kisiasa na kijamii katika Jimbo.

54. Katibu wa Jimbo atakuwa na kazi zifuatazo:

Kazi za Katibu wa Jimbo

(1) Atakuwa mtendaji mkuu na muwajibikaji mkuu wa shughuli zote za kiutendaji za Chama katika Jimbo.

(2) Atatenda kazi zake kwa mashirikiano ya karibu na Mwenyekiti wa Jimbo na Mweka hazina wa Jimbo.

(3) Atakuwa dhamana wa ofisi ya Chama katika Jimbo.

(4) Atahakikisha kuwa nyaraka za Chama katika Jimbo zinatunzwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

(5) Atahakikisha kuwepo na kuhifadhiwa kwa kumbukumbu za vikao vyote vya Chama katika jimbo.

(6) Atakuwa mwajibikaji mkuu wa mambo yote ya fedha na mali za Chama katika Jimbo.

(7) Atatayarisha na kutunza madaftari ya viongozi na wanachama wa Chama pamoja na orodha za wapiga kura katika matawi yote yaliyomo katika Jimbo.

(8) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Jimbo, Kamati ya Utendaji ya Jimbo Mwenyekiti wa Jimbo na Katibu wa Chama wa Wilaya.

55. Mweka Hazina wa Jimbo atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mweka Hazina wa Jimbo

(1) Kutunza mali na fedha za Chama na kutayarisha madaftari ya mahesabu na kuyaweka tayari kwa ajili ya ukaguzi wa ndani na wa nje wakati wote.

(2) Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya kila mwaka ya Chama katika Jimbo.

(3) Kuandaa taarifa za fedha kwa ajili ya vikao vya Chama vya ngazi ya Jimbo na ngazi za juu.

(4) Kubuni miradi ya uchumi katika Jimbo na kuwasilisha mapendekezo yake katika vikao vya Chama vya ngazi ya Jimbo na ngazi za juu.

(5) Kukusanya mapato ya Chama na kufanya malipo yote ya fedha katika Jimbo yatakayoidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni za fedha na taratibu nyingine za Chama zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(6) Kufuatilia ukusanyaji wa mapato na malipo ya fedha katika matawi yaliyomo ndani ya Jimbo hilo.

56. (1) Kiongozi mkuu wa Jimbo anaweza kusimamishwa uongozi na Mkutano Mkuu wa Jimbo.

Kusimamishwa/ Kufukuzwa uongozi kwa Viongozi Wakuu wa Jimbo

(2) Kamati ya Utendaji ya Taifa ndio yenye mamlaka ya kumchukulia hatua za nidhamu Kiongozi Mkuu wa Jimbo, zikiwemo onyo, karipio, karipio kali na hata kumuachisha au kumfukuza uongozi Kiongozi Mkuu yeyote wa Jimbo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii baada ya kupokea mapendekezo ya Mkutano Mkuu wa Jimbo na ya Kamati ya Utendaji ya wilaya endapo tuhuma dhidi ya Kiongozi Mkuu wa Jimbo aliyetuhumiwa zitathibitika.

(3) Endapo Kiongozi Mkuu wa Jimbo ataachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya vijifungu vya (1) na (2) vya Kifungu hiki, basi Kiongozi Mkuu huyo atakuwa na haki ya kukata Rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na kama hataridhika, ataweza kukata Rufaa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama ambao uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Endapo kiongozi mkuu wa jimbo atasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya vijifungu (1) na (2) vya Kifungu hiki mwanachama wa kukaimu nafasi hiyo ya uongozi atachaguliwa kwa mujibu wa vijifungu (1) na (3) vya Kifungu cha 104 cha Katiba hii.

57. 1) Muundo wa Jimbo kwa upande wa Tanzania Bara utakuwa kama ifuatavyo:

2) Jimbo litakuwa na vikao vifuatavyo:-

Muundo wa Jimbo kwa Tanzania Bara

(a) Kamati ya Jimbo

(b) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo

3) Kamati ya Jimbo itakuwa na wajumbe wasiopungua saba (07) na wasiozidi tisa (09) watakaoteuliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa kutokana na mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Wilaya, ambao angalau watatu miongoni mwao watakuwa ni wanawake.

Wajumbe wa Kamati ya Jimbo

4) Endapo Mjumbe wa Kamati ya Jimbo atashindwa kutekeleza wajibu wake kwa sababu yo yote ile, chombo chenye uwezo wa kumuondoa mjumbe huyo kwenye uongozi ni Kamati ya Utendaji ya Taifa tu.

5) Mara baada ya Mjumbe wa Kamati ya Jimbo kondolewa, Kamati ya Utendaji ya Taifa itamteua mwanachama mwengine kujaza nafasi hio, baada ya kupokea mapendekezo kutoka Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

6) Pale ambapo katika wilaya kuna jimbo moja tu, basi hakutakuwa na Kamati ya Jimbo, isipokuwa kwamba kazi ambazo zingepaswa zifanywe na Kamati ya Jimbo zitafanywa na Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

Wajibu wa Kamati ya Jimbo kwa Tanzania Bara

58. (1) Wajibu wa Kamati ya Jimbo ni kuratibu na kusimamia shughuli zote za uchaguzi za viongozi wa serikali za mitaa, madiwani, Mbunge na Rais katika Jimbo.

(2) Kamati ya Jimbo itaongozwa na Mwenyekiti wa Jimbo atakayechaguliwa na Kamati ya Jimbo na ndiye kiongozi mkuu na msemaji mkuu wa shughuli za uchaguzi katika Jimbo

(3) Katibu wa Jimbo atachaguliwa na Kamati ya Jimbo na atakuwa mtendaji mkuu katika usimamizi na uratibu wa shughuli za uchaguzi katika Jimbo.

(4) Mwenyekiti na Katibu wa Jimbo wanaweza kusimamishwa uongozi na Kamati ya Jimbo.

(5) Kamati ya Utendaji ya Taifa ndio yenye mamlaka ya kumuachisha/kumfukuza uongozi Mwenyekiti/ Katibu wa Jimbo baada ya kuzingatia maoni ya Kamati ya Jimbo na Kamati ya Utendaji ya wilaya.

(6) Kiongozi wa Jimbo aliyeachishwa/kufukuzwa uongozi na Kamati ya Utendaji ya Taifa atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambalo uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

Kamati ya Ulinzi na Usalama

59. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo itayokutana angalau mara moja kwa kila baada ya wiki mbili

(2) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo itaongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Jimbo na itakuwa na wajumbe wengine wafuatao:-

(i) Katibu wa Kamati ya Jimbo
(ii) Kamanda wa Blue Guards wa Jimbo
(iii) Mbunge wa Jimbo
(iv) Wanachama wawili wa Jimbo hilo mmoja mwanamke na mmoja mwanamme watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Jimbo baada ya kushauriana na Katibu wa Kamati ya Jimbo

Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama

60. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo ni kama ifuatavyo:-

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama katika eneo zima la Jimbo.

(2) Kukikinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kikodhoofisha Chama katika Jimbo.

(3) Kuhakikisha ulinzi wa Viongozi Wakuu wa Chama wa Jimbo, mali za Chama, majengo ya Chama na shughuli nyingine zote za Chama katika Jimbo.

(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama katika Jimbo.

(5) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo inaweza, kwa maslahi ya Chama kutoa maelekezo ya kiulinzi au maelekezo mengine yoyote inayohisi yanafaa kwa Kamati za Ulinzi za matawi na Kamati hizo zitawajibika kutekeleza maagizo hayo kwa utaratibu uliotolewa na baadae kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Jimbo.

SEHEMU YA TANO

NGAZI YA WILAYA

Wilaya na Muundo wake

61. (1) Katika Katiba hii, wilaya ya Chama itajumuisha maeneo yale ya wilaya katika shughuli za serikali kama itakavyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar au sheria nyingine yeyote iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi kwa ajili hiyo.

(2) Kila wilaya itakuwa na vikao vifuatavyo:-

(a) Mkutano Mkuu wa wilaya
(b) Kamati ya Utendaji ya wilaya
(c) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya

Mkutano Mkuu wa wilaya

62. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa wilaya ambao utakutana kwa vikao vya kawaida mara moja kwa mwaka. Isipokuwa kwamba ikitokea dharura, Kamati ya Utendaji ya wilaya inaweza kuitisha kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa wilaya wakati wowote ule.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya watakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenyekiti wa wilaya.
(b) Katibu wa wilaya.
(c) Wakuu wa vitengo vya Chama vya wilaya.
(d) Wajumbe kumi (10), angalau watatu (3) wakiwa wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kata za wilaya hiyo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(e) Wajumbe kumi na watano (15), angalau watano(5) wakiwa wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila Jimbo la wilaya la Zanzibar kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(f) Wenyeviti na makatibu wa majimbo yaliyomo katika wilaya hiyo.

(g) Wenyeviti na makatibu wa Kata zilizomo katika wilaya hiyo.

(h) Wabunge/Wawakilishi watokanao na Chama wa majimbo ya wilaya hiyo na wale ambao hawana majimbo wanaoishi katika wilaya hiyo.

(i) Kijana mmoja (1) atakayechaguliwa na Jumuiya ya Vijana Kata/Jimbo katika wilaya hiyo kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(j) Mwanamke mmoja (1) aliyechaguliwa na Jumuiya ya Wanawake Kata/ Jimbo katika wilaya hiyo kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(k) Vijana wawili (2), mmoja mwanamke na mmoja mwanamme, kutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Jimbo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(l) Wanawake wawili (2) kutokana na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata kwa Tanzania Bara au wa Jimbo kwa Zanzibar kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(m) Wazee wanne (4), wawili (2) wanawake na wawili (2) wanaume kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kata/Jimbo kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(n) Madiwani watokanao na Chama wa Kata za au Wadi za wilaya hiyo.

(o) Wenyeviti wa halmashauri za wilaya na halmashauri za miji watokanao na Chama wilayani humo.

(p) Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa waishio katika wilaya hiyo.

63. (1) Wajibu wa Mkutano Mkuu wa wilaya utakuwa kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Mkutano Mkuu wa wilaya

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya:-

(i) Taarifa za utendaji wa shughuli za Chama katika wilaya, zikijumlisha taarifa za Kata na majimbo ya wilaya hiyo.

(ii) Taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama katika wilaya za kila mwaka.

(iii) Mapendekezo ya bajeti ya mapato na matumizi ya fedha za Chama ya kila mwaka ya wilaya.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya kuendeleza na kuimarisha Chama katika wilaya.

(v) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo ya uchumi na kijamii katika wilaya.

(vi) Kujenga na kuendeleza udugu wa dhati miongoni mwa wanachama na wananchi wengine katika wilaya.

(b) Kuwa na uamuzi na kauli ya mwisho katika mambo yote ya Chama katika wilaya.

(c) Kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya kiongozi yeyote wa Chama wa wilaya na wa ngazi za chini, pamoja na kusikiliza rufaa kutoka viongozi na wanachama waliochukuliwa hatua za nidhamu na vikao vya chini.

(2) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama Mkutano Mkuu wa wilaya utafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kuwachagua viongozi wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa wilaya.

(ii) Wajumbe kumi na watano (15), angalau watano (05) wakiwa ni wanawake kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya wilaya kutoka miongoni mwao.

(iv) Wajumbe ishirini (20), angalau sita (06) wakiwa ni wanawake, kutoka kila wilaya ya Zanzibar kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa.

(v) Wajumbe wawili (2), angalau mmoja akiwa ni mwanamke, kutoka kila wilaya ya Tanzania Bara kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu waTaifa.

(b) Kuthibitisha mapendekezo ya Mwenyekiti wa wilaya ya Wakuu wa Vitengo vya Chama katika wilaya.

(3) Shughuli nyingine za Mkutano Mkuu wa Wilaya ni pamoja na:-

(a) Kufuatilia masuala yote ya haki za binadaamu na haki za watu katika wilaya.

(b) Kuhakikisha utekelezaji bora wa maamuzi yake na maamuzi ya vikao vya ngazi za juu yake za Chama.

(4) Mkutano Mkuu wa wilaya utaongozwa na Mwenyekiti wa wilaya na asipoweza kuhudhuria kikao chochote kile cha mkutano Mkuu wa wilaya, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya wilaya aliyechaguliwa na kikao hicho, isipokuwa Katibu wa wilaya na, au mkuu wa kitengo katika wilaya. Mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

Kamati ya Utendaji ya wilaya

64. (1) Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya wilaya itakayokutana kwa vikao vya kawaida mara moja kwa mwezi, isipokuwa kwamba pakitokea dharura Kamati ya Utendaji ya wilaya inaweza kukutana katika kikao cha dharura wakati wowote ule kitakapoamuriwa na Mwenyekiti wa wilaya baada ya kushauriana na Katibu wa wilaya.

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya wilaya

(2) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya wilaya watakuwa wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa wilaya

(b) Katibu wa wilaya

(c) Wakuu wa vitengo vya Chama wilaya

(d) Wajumbe kumi na watano (15), angalau watano (05) wakiwa ni wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa wilaya.

(e) Wabunge wawili (2) waliochaguliwa na Wabunge wa wilaya hiyo na Wawakilishi wawili (02) waliochaguliwa na Wawakilishi wa wilaya hiyo watokanao na Chama.

(f) Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa wanaoishi katika wilaya hiyo. Isipokuwa kwamba ikiwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa waishio katika wilaya hiyo wanapindukia watatu (03), basi Wajumbe hao watawachagua Wajumbe wenzao wawili (02) miongoni mwao kuwa Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya wilaya.

(g) Wenyeviti wa halmashauri za wilaya, Miji na Manispaa zilizomo katika wilaya hiyo watokanao na Chama.

(h) Makatibu wa Jumuiya za Vijana, Wanawake na Wazee wa wilaya hiyo.

65. (1) Kamati ya Utendaji ya wilaya itakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

(a) Kusimamia maamuzi ya Mkutano Mkuu wa wilaya na vikao vya ngazi ya juu.

Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya wilaya

(b) Kusimamia uenezi wa itikadi, sera na programu za Chama katika wilaya.

(c) Kuandaa mikakati na mbinu za kuwashawishi wananchi katika Kata na Majimbo ya wilaya hiyo waunge mkono sera, programu na misimamo ya Chama ili kikubalike katika wilaya kwa ujumla.

(d) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa wilaya.

(e) Kutekeleza kazi za kila siku za Chama katika wilaya.

(f) Kutunza, kuhifadhi na kulinda mali, vyombo, nyaraka na mihuri ya Chama katika wilaya.

(g) Kuangalia mapato na matumizi ya Chama katika wilaya.

(h) Kupokea na kuchambua mapendekezo ya vikao vya chini na kuyatolea maamuzi juu ya hatua za kuchukuliwa katika kuyashughulikia.

(i) Kusimamia na kuendesha mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa wanachama na viongozi wa chama katika wilaya.

(j) Kusimamia utimizwaji na kuheshimiwa kwa haki za binaadamu katika wilaya na kuhakikisha kuwa mwananchi yeyote anayeonewa, kunyanyaswa, kukandamizwa na au kudhulumiwa anapata msaada wa Chama katika kutetea na kulinda haki zake.

(k) Kutoa miongozo na kushirikiana na Kamati za Utendaji za Kata na Majimbo katika kuunda vikundi vya kutekeleza miradi ya uchumi na kuendeleza utamaduni na michezo katika eneo la wilaya.

(l) Kushirikiana na vyombo vya dola na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali katika wilaya katika kusimamia na kuendeleza amani na utulivu, kujenga, kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi, za kijamii, na za kiutamaduni katika wilaya.

(m) Kusimamia miradi ya uchumi ya Chama, kuandaa sherehe na tafrija za Chama katika wilaya.

(n) Kushirikiana na vyombo vyengine vya jamii katika usimamizi wa utoaji huduma kwa wazee wasiojiweza, watoto wanaohitaji kusaidiwa na wananchi wengine watakaofikwa na maafa katika wilaya.

(o) Kuwachukulia hatua za nidhamu zikiwemo kuwapa onyo, karipio, karipio kali na hata kuwasimamisha na kuwafukuza uongozi Viongozi Wakuu wa ngazi za chini isipokuwa Viongozi Wakuu wa Jimbo.

(p) Kuwasimamisha uongozi Viongozi Wakuu wa wilaya.

(q) Kujenga na kuimarisha uhusiano mwema na vyama vingine vya siasa katika wilaya.

(2) Wakati wa uchaguzi ndani ya Chama Kamati ya Utendaji ya wilaya itatekeleza majukumu kama yalivyoelezwa katika Kanuni za Uchaguzi zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(3) Wakati wa uchaguzi wa nchi unaoshirikisha vyama vyengine vya siasa Kamati ya Utendaji ya wilaya itafanya shughuli zifuatazo:-

(a) Kusimamia kampeni katika Majimbo, Kata na Matawi ya wilaya hiyo kutegemeana na maelekezo kutoka ngazi ya Taifa.

(b) Kutoa miongozo au kuratibu shughuli za uteuzi wa wasimamizi na, au mawakala wa wagombea wa Chama katika uchaguzi wa nchi, au msimamo wa Chama katika Kura ya Maoni katika vituo vya kujiandikisha na kupigia kura katika wilaya.

(c) Kujiandikisha na kupigia kura katika wilaya kutegemeana na maelekezo kutoka ngazi ya Taifa.

(d) Kusimamia na kuratibu utengenezaji wa madaftari ya chama yenye kumbukumbu za wapiga kura wote wa Majimbo au Kata za wilaya hiyo.

(e) Kusimamia taratibu za uchaguzi wa viongozi wa Chama na viongozi wa kiserikali watokanao na Chama kama itakavoelezwa katika Kanuni za uchaguzi kama zilivyotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(4) Kamati ya Utendaji ya wilaya itaongozwa na Mwenyekiti wa wilaya na asipoweza kuhudhuria kikao chochote kile cha Kamati ya Utendaji ya wilaya, kikao hicho kitaongozwa na mjumbe mwingine yeyote wa kikao aliyechaguliwa na kikao chenyewe, isipokuwa Katibu wa wilaya au mkuu wa kitengo cha chama cha wilaya. Mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

66. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya itayokutana angalau mara moja kwa kila mwezi.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya

(2) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya itaongozwa na Mwenyekiti wa wilaya na itakuwa na wajumbe wengine wafuatao:-

(i) Katibu wa wilaya.
(ii) Kamanda wa Blue Guards wa wilaya.
(iii) Mbunge mmoja aliyechaguliwa na Wabunge wa majimbo na wale wanaoishi katika wilaya hiyo.
(iv) Mwakilishi mmoja aliyechaguliwa na Wawakilishi wa majimbo na wale wanaishi katika wilaya hiyo.
(v) Wanachama wawili, mmoja mwanamke na mmoja mwanamme watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa wilaya baada ya kushauriana na Katibu wa wilaya kutokana na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

67. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ni kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama katika eneo zima la wilaya.

(2) Kukikinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kikodhoofisha Chama katika wilaya.

(3) Kuhakikisha ulinzi wa Viongozi Wakuu wa Chama wa wilaya, mali za Chama, majengo ya Chama na shughuli nyingine zote za Chama katika wilaya.

(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama katika wilaya.

(5) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya inaweza, kwa maslahi ya Chama kutoa maelekezo ya kiulinzi au maelekezo mengine yoyote inayohisi yanafaa kwa Kamati za Ulinzi za ngazi za chini, na Kamati hizo zitawajibika kutekeleza maagizo hayo kwa utaratibu uliotolewa na baadae kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya

68. (1) Kutakuwa na vitengo vya Chama katika wilaya ambayo idadi na majina yake yataamuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Vitengo vya Chama vya wilaya

(2) Kila kitengo kitaongozwa na Mkuu wa kitengo atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa wilaya kwa kushauriana na Katibu wa wilaya na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa wilaya.

(3) Majukumu ya vitengo vya Chama katika wilaya yataainishwa katika Kanuni

zitakazotungwa mara kwa mara na Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa ajili hiyo na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(4) Kila Mkuu wa kitengo wa wilaya atasimamia utekelezaji wa majukumu ya kitengo chake kama yalivyoainishwa na Kanuni zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

69. Kutakuwa na Viongozi Wakuu wafuatao wa Chama katika wilaya:-

Viongozi Wakuu wa Wilaya

(1) Mwenyekiti wa wilaya.

(2) Katibu wa wilaya.

70. Mwenyekiti wa wilaya atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Mwenyekiti wa wilaya

(1) Ndiye atayekuwa Kiongozi Mkuu wa shughuli za Chama katika wilaya na atakuwa msemaji mkuu wa Chama katika wilaya.

(2) Ataongoza vikao vyote vya Mkutano Mkuu, Kamati ya Utendaji ya wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya.

(3) Atakuwa na kura ya uamuzi endapo katika kikao anachokiongoza kura za wajumbe zitafungana.

(4) Atakiwakilisha Chama katika shughuli za kisiasa na kijamii katika wilaya.

(5) Atajenga uhusiano mzuri na viongozi wa vyama vingine vya siasa katika wilaya.

(6) Akishauriana na katibu wa wilaya atateua wakuu wa vitengo vya Chama katika wilaya na kisha kuwapeleka mbele ya Mkutano Mkuu wa wilaya kwa kuthibitishwa.

(7) Mwenyekiti wa wilaya ambayo ni Makao Makuu ya Mkoa atakiwakilisha Chama katika shughuli za kiserikali na kijamii katika Mkoa huo.

71. (1) Katibu wa Chama wa wilaya atateuliwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa, na atakuwa na kazi zifuatazo:-

Kazi za Katibu wa wilaya

(a) Atakuwa katibu wa Mkutano Mkuu wa wilaya na Kamati ya Utendaji ya wilaya.

(b) Atakuwa mtendaji mkuu wa Chama na mwajibikaji mkuu wa shughuli zote za kiutendaji za Chama katika wilaya.

(c) Atatenda kazi zake kwa mashirikiano ya karibu na Mwenyekiti wa wilaya na wakuu wa vitengo vya Chama katika wilaya.

(d) Atakuwa dhamana wa ofisi ya Chama katika wilaya.

(e) Atahakikisha kwamba nyaraka za Chama katika wilaya zinatunzwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

(f) Atahakikisha kuwepo na kuhifadhiwa kwa kumbukumbu za vikao vyote vya Chama katika wilaya.

(g) Atakuwa mwajibikaji mkuu wa mambo yote ya fedha na mali za Chama katika wilaya.

(h) Atatayarisha na kutunza takwimu zote zinazohusu idadi ya wanachama na idadi ya wapiga kura katika wilaya, na kuwa na kumbukumbu za viongozi wa Majimbo, Kata na Matawi ya wilaya hiyo.

(i) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa wilaya, Kamati ya Utendaji ya wilaya, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Chama, Mwenyekiti wa wilaya au maagizo mengine yeyote atakayopewa na kikao chochote cha ngazi ya Taifa.

(2) Katibu wa wilaya ambaye wilaya yake ndiyo Makao Makuu ya Serikali ya Mkoa atakuwa pia na wajibu ufuatao:-

(a) Atakuwa kiungo baina ya Makatibu wa wilaya zilizomo katika Mkoa, isipokuwa katibu wa wilaya hiyo hatakuwa na uwezo wa kuingilia kazi za wilaya nyingine za Mkoa huo.

(b) Atakuwa kiungo baina ya Makao Makuu ya Chama na ofisi za wilaya za Chama za Mkoa huo pale itakapohitajika.

Miradi ya Vitengo

72. Kila kitengo kilichoanzishwa chini ya kifungu 68 cha Katiba hii, kinaweza kubuni miradi yake pamoja na kuweka mikakati yake mingine kwa ajili ya kuboresha kitengo hicho, mradi tu idhini ya kufanya hivyo iwe imepatikana kutoka kwa Kamati ya Utendaji ya wilaya na kwa kuzingatia Kanuni zilizowekwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

73. (1) Kamati ya Utendaji ya wilaya inaweza kumsimamisha uongozi Mwenyekiti wa wilaya. Mkutano Mkuu wa wilaya utabidi kuthibitisha kusimamishwa uongozi

Kusimamishwa/ Kufukuzwa uongozi Mwenyekiti wa wilaya

Mwenyekiti wa wilaya na hata kumpigia kura ya kutokuwa na imani naye katika kipindi kisichozidi siku 90 tangu tarehe ya kusimamishwa kwake.

(2) Endapo Mkutano Mkuu umepiga kura ya kutokuwa na imani na Mwenyekiti wa wilaya, itahesabiwa kuwa Mwenyekiti huyo ameachishwa uongozi.

(3) Mwenyekiti wa wilaya aliyeachishwa uongozi na Mkutano Mkuu wa wilaya anaweza kukata rufaa kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa, na kama hakuridhika anaweza kukata rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambalo uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Endapo Mwenyekiti wa wilaya atasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi, Mkutano Mkuu wa wilaya utamchagua Mjumbe mmoja asiyekuwa Katibu wa wilaya au Mkuu wa Kitengo katika wilaya kuwa Mwenyekiti wa muda hadi pale atapochaguliwa Mwenyekiti wa wilaya mwengine kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Katiba hii na Kanuni za Uchaguzi zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

74. (1) Uwezo wa kumsimamisha, kumuachisha au kumfukuza uongozi Katibu wa wilaya umo mikononi mwa Kamati ya Utendaji ya Taifa Katibu wa wilaya aliyechukuliwa moja au zaidi ya hatua zilizoainishwa Katika kijifungu hiki anaweza kukata rufaa kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambalo uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

Kusimamishwa/ Kufukuzwa uongozi Katibu wa wilaya

(2) Endapo Katibu wa wilaya amechukuliwa hatua kwa mujibu wa kijifungu cha (1) cha Kifungu hiki, Kamati ya Utendaji ya Taifa itamteua Mkuu wa Kitengo cha Mipango na Chaguzi kuwa Kaimu Katibu wa wilaya hadi hapo Katibu wa wilaya mpya atakapoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

SEHEMU YA SITA

NGAZI YA TAIFA

Eneo la Chama Kitaifa

75. Eneo la Chama ngazi ya Taifa ni eneo lote la Tanzania Bara na Zanzibar kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge au Baraza la Wawakilishi.

Muundo wa Chama Kitaifa

76. Kitaifa Chama kitakuwa na vikao vinne vifuatavyo:

(1) Mkutano Mkuu wa Taifa.

(2) Baraza Kuu la Uogozi la Taifa.

(3) Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(4) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa

Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa

77. (1) Kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Taifa utakaokutana kwa vikao vya kawaida mara moja baada ya kila miezi sitini (60). Mkutano Mkuu wa Taifa ndio chombo kikuu cha Chama chenye maamuzi ya mwisho ya shughuli zote za Chama nchini.

(2) Mkutano Mkuu wa Taifa wa dharura unaweza ukaitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa endapo itatokea sababu muhimu na nzito itakayofanya ulazima wa kuitishwa kwa Mkutano Mkuu huo.

(3) Kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa Taifa kitafanyika pia pale ambapo zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Zanzibar na zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Tanzania Bara watataka kwa maandishi kupitia Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuitishwa kwa kikao hicho.

(4) Iwapo Mkutano Mkuu wa Taifa utaitishwa kwa masharti ya kijifungu cha (3) cha Kifungu hiki, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litalazimika kuitisha kikao cha dharura cha Mkutano Mkuu wa Taifa katika siku zisizozidi mia moja na themanini (180) tangu kupokea ombi la wajumbe hao.

(5) Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa halali iwapo zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Tanzania Bara na zaidi ya nusu ya wajumbe wake kutoka Zanzibar watahudhuria.

(6) Maamuzi yatakayofanywa na Mkutanno Mkuu wa Taifa yatahesabiwa kuwa maamuzi halali ikiwa zaidi ya nusu ya wajumbe waliohudhuria watayaunga mkono.

(7) Maamuzi muhimu yatahesabiwa kuwa maamuzi halali ya Mkutano Mkuu wa Taifa ikiwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe kutoka Tanzania Bara waliohudhuria, na zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe kutoka Zanzibar waliohudhuria watayaunga mkono maamuzi hayo.

(8) Kwa madhumuni ya kijifungu cha (7) cha Kifungu hiki maamuzi muhimu ni pamoja na:-

Maamuzi muhimu ya Chama

(a) Kuvunja Chama.

(b) Kubadilisha jina la Chama.

(c) Kuunganisha Chama na chama au vyama vya siasa vingine.

(d) Kuwasimamisha, kuwaachisha au kuwafukuza uongozi na/au uanachama Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Chama pamoja na viongozi wengine wa Kitaifa kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba hii.

(e) Kuwaachisha, kuwafukuza uanachama Rais na/au Makamu Rais wa Jamhuri ya Muungano na Rais wa Zanzibar anayetokana na Chama.

(f) Kupitisha, kurekebisha au kubadilisha Katiba hii au kifungu chochote cha Katiba hii.

(g) Kupitisha, kurekebisha au kubadilisha itikadi ya Chama na.

(h) Mambo mengine yoyote ambayo Mkutano Mkuu wa Taifa kwa masharti yale yale ya kijifungu cha (7) cha Kifungu hiki utaamua kuwa ni maamuzi muhimu.

78. (1) Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wake wafuatao:-

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama wa Taifa

a) Mwenyekiti wa Taifa.
b) Makamu Mwenyekiti.
c) Katibu Mkuu.
d) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na Chama hiki.
e) Rais wa Zanzibar, Makamo wa Kwanza au Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar kutokana na Chama hiki.

f) Manaibu Katibu Mkuu.
g) Wajumbe wote wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.
h) Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutokana na Chama hiki.
i) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kutokana na Chama hiki.
j) Wenyeviti wa wilaya zote za Tanzania Bara na za Zanzibar.
k) Makatibu wa wilaya zote za Tanzania Bara na za Zanzibar.
l) Wajumbe wawili, mmoja akiwa ni mwanamke, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa kila wilaya ya Tanzania Bara.
m) Wajumbe ishirini (20), angalau sita (06) wakiwa ni wanawake, waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kila Wilaya ya Zanzibar.
n) Wajumbe kumi na watano (15), wajumbe tisa (09) kutoka Tanzania Bara, angalau watatu (03) wakiwa ni wanawake, na wajumbe sita (06) kutoka Zanzibar, angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti,
o) Wajumbe walemavu watano, watatu (03) kutoka Tanzania Bara, na wawili (02) kutoka Zanzibar walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, isipokuwa wajumbe wasiopungua wawili miongoni mwao wawe ni wanawake.
p) Mwenyekiti wa Taifa na Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa kila Jumuiya ya Chama
q) Katibu Mtendaji na Naibu Katibu Mtendaji wa kila Jumuiya ya Chama.
r) Wajumbe kumi (10); sita (06) angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake kutoka Tanzania Bara, na wajumbe wanne (04), angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake kutoka Zanzibar waliochaguliwa na Baraza la Taifa la Jumuiya ya Vijana ya Chama
s) Wajumbe kumi (10); sita (06) angalau wawili (2) wakiwa ni wanawake kutoka Tanzania Bara, na wajumbe wanne (04) angalau wawili wakiwa ni wanawake kutoka Zanzibar waliochaguliwa na Baraza la Taifa la Jumuiya ya Wazee.
t) Asilimia kumi (10%) ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka Tanzania Bara, na asilimia kumi (10%) ya Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka Zanzibar waliochguliwa na Baraza la Taifa la Jumuiya ya Wanawake ya Chama.

(2) Endapo nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile basi Mamlaka iliyomchagua au kumteua mjumbe huyo itaijaza nafasi hiyo kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika Kanuni za Uchaguzi.

79. Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa kama ifuatavyo:-

(1) (a) Kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya:-

Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Taifa

(i) Taarifa za fedha za kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.
(ii) Taarifa za mkaguzi wa nje wa mahesabu ya Chama ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.

(iii) Taarifa ya mapato na matumizi ya Chama ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano kwa pamoja.

(iv) Mapendekezo ya mipango ya maendeleo ya Chama na serikali inayoendeshwa na Chama.

(v) Taarifa za utekelezaji wa itikadi na sera za Chama kutoka viongozi wa Chama na Viongozi wa serikali inayoendeshwa na Chama na, au viongozi wa Wabunge na Wawakilishi wa Chama.

(b) Kutunga, kusahihisha au kurekebisha Katiba ya Chama pale ambapo Mkutano Mkuu utaona inafaa.

(c) Kuthibitisha itikadi na sera za Chama za kiuchumi, kijamii maendeleo na sera nyingine zilizotungwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, na kupokea, kujadili na kutoa maamuzi juu ya taarifa ya utekelezaji wa itikadi na sera hizo.

(d) Kubuni, kufanya tathmini na kutoa maelekezo juu ya mipango ya kukiimarisha Chama nchini kote.

(e) Kujenga udugu wa dhati miongoni mwa watanzania wote pamoja na wananchi wa nchi jirani na nchi nyingine duniani.

(f) Kuthibitisha au kutengua uamuzi wowote uliotolewa na kikao chochote cha chini au kiongozi yeyote wa Chama.

(g) Kupokea Rufaa na kutoa maamuzi ya mwisho juu ya Rufaa hizo kutoka viongozi au wanachama waliochukuliwa hatua za nidhamu na vikao vya chini, isipokuwa pale ambapo Katiba hii imeelekeza vingine.

(h) Bila ya kuathiri Kifungu 77 (7) na (8) cha Katiba hii kutoa uamuzi wa kubadili jina la Chama, kuunganisha Chama hiki na chama au vyama vyengine vya siasa nchini, au hata kukivunja Chama.

(i) Wakati wa uchaguzi wa ndani ya Chama; Mkutano Mkuu wa Taifa utafanya shughuli zifuatazo:-

(j) Kuchagua Mwenyekiti wa Taifa.

(k) Kuchagua Makamu Mwenyekiti.

(l) Kuchagua Katibu Mkuu.

(m) Kuchagua kutoka miongoni mwa wajumbe wake, wajumbe arobaini na watano (45), angalau kumi na tano (15) wakiwa ni wanawake, kuingia katika Baraza Kuu la Uongozi la Taifa; ambapo ishirini na watano (25), angalau tisa (09) wakiwa ni wanawake kutoka Tanzania Bara na ishirini (20), angalau sita (6) wakiwa ni wanawake kutoka Zanzibar.

(n) Kuthibitisha wajumbe kumi na watano (15);ambapo tisa (09), angalau watatu (03) wakiwa ni wanawake kutoka Tanzania Bara, na sita (06) angalau wawili (02) wakiwa ni wanamke kutoka Zanzibar, walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka Miongoni mwa wanachama wajasiri wa Chama.

(o) Kuthibitisha wajumbe walemavu watano (05), watatu (03) kutoka Tanzania Bara, na wawili (02) kutoka Zanzibar walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti kuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwa wanachama wajasiri wa Chama.

(p) Wakati wa uchaguzi wa nchi unaohusisha vyama vyengine vya siasa nchini, Mkutano Mkuu wa Taifa utatekeleza majukumu yake kama yatavyowekwa katika Kanuni za Uchaguzi wa Chama zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Mkutano Mkuu kuchukua hatua za kinidhamu

(2) (a) Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza kuchukua hatua za kinidhamu zozote zile zikiwemo kumuachisha au kumfukuza uongozi au uanachama au yote mawili Kiongozi Mkuu wa Kitaifa au Kiongozi wa Kitaifa yeyote wa Chama au Kiongozi yeyote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar atokanaye na Chama hiki.

(b) Mwanachama mwengine yoyote naye pia anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu zilizoelezewa katika kijifungu kidogo cha (a) cha kijifungu cha (2) cha kifungu hiki.

(3) Mkutano Mkuu wa Taifa utaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa na asipoweza kuhudhuria kikao chochote, kikao hicho kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti, na ikiwa Makamu Mwenyekiti naye hataweza kuhudhuria kikao hicho, kikao kitamchagua mjumbe mmoja wa Mkutano Mkuu wa Taifa mwenye uzoefu mkubwa asiyekuwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu au mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa kuongoza kikao hicho na mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

Baraza Kuu la Uonozi la Taifa

80. (1) Kutakuwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litakalokutana kwa vikao vyake vya kawaida kila baada ya miezi minne isipokuwa kwamba pakitokea dharura Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kukutana katika kikao cha dharura wakati wowote Kamati ya Utendaji ya Taifa au Mwenyekiti wa Taifa kwa kushauriana na Makamu Mwenyekiti wataona umuhimu wa kuitishwa kwa kikao cha dharura na kuamuru kiitishwe.

Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa

81. (1) Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa watakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mwenyekiti wa Taifa
(ii) Makamo Mwenyekiti wa Taifa
(iii) Katibu Mkuu
(iv) Manaibu Katibu Mkuu
(v) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wanaotokana na Chama.
(vi) Rais na Makamu wa Rais wa Zanzibar wanaotokana na Chama.
(vii) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa.
(viii) Wajumbe arobaini na watano (45), ishirini na watano (25) kutoka Tanzania Bara, ambao angalau wanane (08) watakuwa ni wanawake, na wajumbe ishirini (20) kutoka Zanzibar, ambao angalau sita (06) watakuwa ni wanawake waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa kutoka miongoni mwao kwa kufuata tararibu zilizozowekwa katika Kanuni za Uchaguzi kama zilivyotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na Kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.
(ix) Wajumbe watano (05), watatu kutoka Tanzania Bara na wawili (02) kutoka Zanzibar watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti Chama kutokana na wanachama wajasiri wa Chama, isipokua ijulikane tu wajumbe wasiopungua asilimia thelathini (30%) ya Wajumbe hao wa kuteuliwa watakuwa ni wanawake.
(x) Wajumbe walemavu wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, ambapo mmoja atakuwa mwanamke na mwengine atakuwa mwanamme, kutokana na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa au wanachama wajasiri wa Chama.
(xi) Mwenyekiti wa kila Jumuiya ya Chama pamoja na Mjumbe mmoja aliyechaguliwa na Baraza la Taifa la kila Jumuiya ya Chama.
(xii) Kiongozi wa kambi ya wabunge wa Chama katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.
(xiii) Kiongozi wa kambi ya Wawakilishi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

(2) Endapo nafasi ya Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa itakuwa wazi kwa sababu yoyote ile, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litaijaza nafasi hiyo kutoka kundi ambalo Mjumbe ambaye nafasi yake iko wazi alitokea.

(3) Maamuzi yote ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa yatafikiwa kwa maafikiano au kwa wingi wa kura.

(4) Maamuzi muhimu yatahesabiwa kuwa halali ikiwa zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe kutoka Tanzania Bara na zaidi ya theluthi mbili(2/3) ya wajumbe kutoka Zanzibar watayaunga mkono.

(5) Kwa madhumuni ya kijifungu cha (4) cha kifungu hiki maamuzi muhimu yatahusu mambo yote yaliyoorodheshwa katika kifungu cha 77 (8) cha Katiba hii na kama yatakavyorekebishwa mara kwa mara.

82. (1) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litakuwa na wajibu kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa

(a) Kutoa ufafanuzi wa itikadi za Chama zilizobuniwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.
(b) Kutunga sera na Ilani za Uchaguzi za Chama.
(c) Kusimamia utekelezaji bora wa maamuzi na maelekezo mbalimbali ya Mkutano Mkuu wa Taifa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.
(d) Kutoa miongozo na maelekezo ya kisiasa kwa ngazi za chini za Chama katika kuhakikisha utekelezaji bora wa Katiba hii, itikadi ya uliberali, imani, maadili na sera za Chama.
(e) Kulinda na kuendeleza heshima ya Chama na serikali zote halali za nchi.
(f) Kuanzisha, kufuta au kuongeza Kurugenzi za Chama za Taifa, na vitengo vya Chama vya wilaya na kuziunganisha au kuzitenganisha inapohitajika pamoja na kupanga majukumu na kazi za Kurugenzi na Vitengo hivyo, ikiwa ni pamoja na kuiongezea, au kuipunguzia majukumu Kurugenzi au Kitengo cho chote kile.
(g) Kujenga na kuimarisha uhusiano mwema na vyama vingine vya siasa vya ndani na nje ya nchi, vyenye kupenda demokrasia ya kweli,
(h) Kuhamasisha kuheshimiwa kwa haki za binaadamu na haki za watu kama zilivyotangazwa na Matamko ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika.
(i) Kuendeleza amani na utulivu na kupinga vitendo vyo vyote vinavyoashiria utawala wa mabavu.
(j) Kuzingatia maombi ya vyama vingine vya siasa na, au jumuiya za vyama vya siasa vya ndani na nje ya nchi vitakavyoomba kushirikiana au kujiunga na Chama hiki.
(k) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Taifa.

(l) Kuthibitisha Kanuni zote zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(m) Kuwachukulia hatua za nidhamu viongozi na wanachama wanaoshutumiwa kwa makosa mbalimbali kwa kufuata masharti ya Katiba hii na Kanuni zitakazotungwa mara kwa mara kwa mujibu wa Katiba hii.

(2) Katika kusimamia vyema shughuli za utendaji katika Chama, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa:-

(a) Litafuatilia kwa karibu shughuli zote za Makao Makuu na Ofisi Kuu ya Chama na kutoa maelekezo ipasavyo.

(b) Litapokea na kujadili taarifa za utendaji kutoka kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa, ngazi za wilaya, Majimbo, Kata na Matawi na kutoa miongozo mbalimbali ya kufanikisha shughuli za Chama nchini kote.

(c) Litasimamia na kufuatilia kwa ukaribu kazi za Kurugenzi zote za Chama.

(d) Litateua Bodi ya Wadhamini ya Chama.

(e) Litateua Mkaguzi wa Ndani wa Mahesabu ya Chama.

(f) Litathibitisha Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi wa Kurugenzi za Chama walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Mkutano Mkuu wa Taifa au wanachama wajasiri wa Chama, hata kama wajasiri hao si Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa au Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(g) Litahakikisha kwamba alama muhimu za Chama zinasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

(h) Litahakikisha utekelezaji bora na wa dhati wa masharti yote ya sheria za nchi zinazohusu usajili wa vyama vya siasa, uendeshaji wa vyama vya siasa na mapato na matumizi ya fedha na mali nyingine za Chama.

(i) Litapokea mialiko kutoka vyama rafiki vya ndani na nje ya nchi.

(3) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litaongozwa na Mwenyekiti wa Taifa, na asipoweza kuhudhuria kikao hicho, kikao hicho kitaongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama, na ikiwa Makamu Mwenyekiti naye hataweza kuhudhuria kikao hicho, kikao kitamchagua mjumbe mmoja wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa asiyekuwa Katibu Mkuu wa Chama au mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa kuongoza kikao hicho na mjumbe huyo atakuwa mwenyekiti wa muda wa kikao hicho tu.

83. (1) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuwasimamisha uongozi Viongozi Wakuu wa Chama wa Taifa wafuatao:-

Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuchukua hatua za kinidhamu

(a) Mwenyekiti wa Taifa .
(b) Makamu Mwenyekiti.
(c) Katibu Mkuu

(2) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuwasimamisha uanachama Viongozi Wakuu wa serikali wa Taifa watokanao na Chama wafuatao:-

(a) Rais wa Jamhuri ya Muungano.
(b) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.
(c) Rais wa Zanzibar.
(d) Makamu wa Rais wa Zanzibar

(3) Endapo kiongozi yeyote aliyetajwa katika vijifungu vya (1) na (2) vya Kifungu hiki atasimamishwa Uongozi au uanachama, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litalazimika kufikisha mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa, taarifa ya kusimamishwa uongozi au uanachama kiongozi huyo kwa haraka kama itakavyowezekana. Kwa vyovyote vile taarifa hiyo; ikieleza sababu za kuchukuliwa kwa hatua hiyo na mapendekezo ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, itafikishwa mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa katika kipindi kisichozidi siku tisini (90) tangu uamuzi huo uchukuliwe.

(4) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuchukua hatua za nidhamu zilizoainishwa katika kijifungu (5) cha Kifungu hiki dhidi ya viongozi watokanao na Chama wafuatao:-

(a) Naibu Katibu Mkuu.
(b) Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.
(c) Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini.
(d) Waziri Mkuu na/au Kiongozi wa Upinzani Bungeni.
(e) Makamu wa Rais wa Zanzibar na/au Kiongozi wa Upinzani katika Baraza la Wawakilishi.
(f) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.
(g) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.
(h) Mwenyekiti wa Jumuiya ya Chama.
(i) Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Chama.
(j) Kiongozi mwengine yeyote wa chama na Serikali wa ngazi yeyote ile.

(5) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuchukua hatua za nidhamu zifuatazo dhidi ya kiongozi yeyote aliyetajwa katika kijifungu (4) cha Kifungu hiki:-

(a) Kutoa onyo kwa maandishi au
(b) Kutoa karipio au karipio kali kwa maandishi au
(c) Kumsimamisha au kumfukuza uanachama.

(6) Bila ya kuathiri vijifungu (4) na (5) vya Kifungu hiki, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa halitalazimika kuchukua hatua hizo za nidhamu dhidi ya kiongozi yeyote yule kwa mpangilio uliowekwa katika kijifungu cha (5) cha kifungu hiki, bali litaweza kuchukua hatua yoyote ile miongoni mwa hizo au zaidi ya hatua moja kwa pamoja kutegemea uzito wa kosa alilotuhumiwa nalo kiongozi baada ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuridhika kuwa kiongozi huyo amelitenda kosa hilo.

(7) Endapo Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litapomvua madaraka mjumbe wa Bodi ya Wadhamini au Naibu Katibu Mkuu, litalazimika kumteua mjumbe mwingine wa Bodi ya Wadhamini au kumchagua Naibu Katibu Mkuu mwingine kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii katika kikao chake kinachofuata ikiwa muhusika hakukata Rufaa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa.

Kamati ya Utendaji ya Taifa

84. (1) Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa ambayo itakutana mara moja kwa kila miezi miwili. Isipokuwa kwamba ikitokea dharura Kamati hiyo inaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote ambao Mwenyekiti wa Kamati hiyo ataamuru hivyo.

(2) Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa

(a) Katibu Mkuu.
(b) Manaibu Katibu Mkuu.
(c) Wakurugenzi wa Kurugenzi za Chama za Taifa.
(d) Manaibu Wakurugenzi wa Kurugenzi za Chama Taifa.
(e) Katibu na Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama.
(f) Makatibu Watendaji wa Jumuiya zote za Chama.

(3) (a) Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa au Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au mwanachama mwengine yoyote yule anaweza kuteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, baada ya kushauriana na Makamo Mwenyekiti kuwa Mjumbe Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(b) Pale ambapo mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa; ambaye kabla ya kuteuliwa kwake hakuwa mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, ataacha kuwa mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa kwa sababu yoyote ile, basi atasita mara moja kuwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(4) Katibu Mkuu ataongoza vikao vyote vya Kamati ya Utendaji ya Taifa na asipoweza kuhudhuria kikao chochote cha Kamati ya Utendaji ya Taifa, kikao hicho kitaongozwa na Naibu Katibu Mkuu anayemfuata Katibu Mkuu kwa madaraka, na kama naye hayupo kikao hicho kitaongozwa na Naibu Katibu Mkuu mwingine. Kama wote hawapo kwa dharura, basi wajumbe waliopo katika kikao hicho watamteua Mkurugenzi mmoja mwandamizi miongoni mwao kuongoza kikao hicho tu.

85. Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Taifa utakuwa kama ifuatavyo:-

Wajibu wa Kamati ya Utendaji ya Taifa

(1) Kuhakikisha kuwa Chama wakati wote kinakwenda na wakati katika mahusiano, mawasiliano na utendaji wa shughuli za Chama kisayansi na uyakinifu.

(2) Kutekeleza maagizo yote ya Mkutano Mkuu wa Taifa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(3) Kutekeleza kazi za kila siku za Chama ngazi ya Taifa.

(4) Kutunza, kuhifadhi na kulinda mali, vyombo, nyaraka na mihuri ya Chama katika ngazi ya Taifa.

(5) Kuandaa agenda za Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na kutayarisha na kuhifadhi mihutasari ya vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na vya Kamati ya Utendaji ya Taifa yenyewe, na kuwasilisha taarifa ya yatokanayo kutokana na utekelezaji wa maamuzi ya kikao kilichohusika kilichopita.

(6) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Chama na kufikisha taarifa ya mambo hayo katika kila kikao cha Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(7) Kuandaa na kuendesha mafunzo ya siasa, uongozi na utendaji kwa viongozi na watendaji wa Chama.

(8) Kupokea na kuchambua mapendekezo ya vikao vya chini na kuyafanyia kazi ipasavyo na pia kufikisha kwa vikao vya chini maamuzi na maelekezo ya vikao vya Taifa.

(9) Kuwateua na kuwapangia vituo vya kazi Makatibu wa wilaya.

(10) Kuwateua na kuwapangia kazi watendaji na watumishi wa Chama wa Makao Makuu, Ofisi Kuu na Ofisi nyingine zilizoanzishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(11) Kumsimamisha kazi Mkurugenzi au Naibu mkurugenzi kwa utovu wa nidhamu au kushindwa kazi na kulitaarifu Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa uamuzi wa mwisho.

(12) Kumsimamisha, kumuachisha au kumfukuza uongozi Kiongozi ye yote wa wilaya, Jimbo na Kata kutokana na makosa ya kinidhamu, uchochezi wa migogoro na ubadhirifu wa fedha na mali za chama au kushindwa kazi.

(13) Kuisimamisha kazi, kuiachisha kazi ua kuifukuza kazi Kamati ya Utendaji ya wilaya, Jimbo au Kata kwa kushindwa kufanya kazi za Chama, kushabikia migogoro miongoni mwa viongozi na ubadhirifu wa fedha na mali za chama.

(14) Endapo hatua zilizoainishwa katika vijifungu 12 na 13 vya Kifungu hiki zitachukuliwa, Kamati ya Utendaji ya Taifa itawajibika kuweka kaimu wa kiongozi aliyesimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa, na pia kuweka uongozi wa muda kuchukua nafasi ya uongozi uliosimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuhusu muda wa kukaimu.

(15) Kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa baadhi ya vifungu vya Katiba hii, na baadae kuziwasilisha mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama Taifa

86. (1) Kutakuwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa ya Chama ambayo itafanya vikao vya kawaida mara moja kila baada ya miezi minne. Kikao cha dharura cha Kamati ya Ulinzi na Usalama kinaweza kufanyika panapotokea haja na Mwenyekiti wa Taifa kuamuru hivyo.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama watakuwa kama wafuatavyo:-

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa

(a) Mwenyekiti wa Taifa
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu Mkuu.
(d) Manaibu Katibu Mkuu.
(e) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watokanao na Chama.
(f) Rais wa Zanzibar atokanaye na Chama.
(g) Waziri Mkuu au Kiongozi wa Upinzani rasmi atokanaye na Chama, au Kiongozi wa Wabunge wa CUF katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.
(h) Makamu wa Rais au kiongozi wa wawakilishi wa CUF katika Baraza la Wawakilishi atokanaye na Chama
(i) Waziri wa Ulinzi au Waziri kivuli wa Ulinzi atokanaye na Chama.
(j) Waziri wa Mambo ya nje au Waziri kivuli wa Mambo ya Nje atokanaye na Chama.
(k) Katibu na Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama.
(l) Waziri wa Serikali ya Mapinduzi au Waziri Kivuli wa Zanzibar anayeshughulikia Idara Maalum (Vikosi) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(m) Wajumbe wengine wane (4), ambapo wawili (2), angalau mmoja (1) akiwa ni mwanamke kutoka Tanzania Bara na wawili (2), angalau mmoja (1) akiwa ni mwanamke kutoka Zanzibar, walioteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au wanachama wajasiri wa Chama.

(3) Mwenyekiti wa Taifa ataongoza vikao vyote vya Kamati ya Ulinzi na Usalama, na asipoweza kuhudhuria kikao chochote kile Makamu Mwenyekiti ataongoza kikao hicho. Endapo wote wawili hawatakuwapo katika kikao chochote kile Katibu Mkuu wa Chama atakuwa Mwenyekiti wa muda na ataongoza kikao hicho tu.

87. Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa utakuwa kama ifuatavyo:

Wajibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama ya Taifa

(1) Kuhakikisha usalama wa Chama nchini kote.
(2) Kukikinga Chama kutokana na njama za ndani na nje ya Chama za kukisambaratisha au kukidhoofisha.
(3) Kuhakikisha ulinzi na usalama wa viongozi wakuu wa Chama, mali za Chama, majengo ya Chama, na shughuli zote za Chama.
(4) Kuratibu shughuli za vijana walinzi wa Chama, Makao Makuu, Ofisi Kuu na katika Taifa kwa jumla.
(5) Kuteua Makamanda wa Blue Guards wa Wilaya kufuatana na mapendekezo ya Kamati za Ulinzi na Usalama za Wilaya kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa.
(6) Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa inaweza kwa maslahi ya Chama kutoa maelekezo ya kiulinzi au maelekezo mengine yoyote inayohisi yanafaa kwa Kamati za Ulinzi za ngazi za chini na Kamati hizo zitawajibika kutekeleza maagizo hayo kwa utaratibu uliotolewa na baadae kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa.

88. (1) Kutakuwa na Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama ambaye kwa wadhifa wake atakuwa ni mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa. Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama atateuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, au wanachama wajasiri wa Chama.

Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa

(2) Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama atakuwa na majukumu yafuatayo:-

(a) Atakuwa mtendaji mkuu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama.

(b) Atatekeleza kazi zote atakazopewa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu.

(c) Atakuwa katibu wa vikao vyote vya Kamati ya Ulinzi na Usalama na atatunza na kuhifadhi kumbukumbu za vikao hivyo.

(d) Atakuwa msimamizi mkuu wa shughuli zote za walinzi wa Chama.

Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa

89. Kutakuwa na Naibu katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye kwa wadhifa wake atakuwa pia ni mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa na atateuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au wanachama wajasiri wa Chama.

(1) Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama atamsaidia Katibu wa Kamati hiyo katika shughuli zake zote alizopewa na kwa masharti ya Katiba hii, au atafanya kazi nyingine zozote kama atakavyoagizwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu au Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa,

(2) Atakuwa Kaimu Katibu wa Kamati hiyo pale ambapo Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama atakuwa hayupo, au hawezi kutekeleza Majukumu yake kwa sababu yoyote ile.

(3) Endapo Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama atatokea upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama atatokea upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA SABA

VIONGOZI WA KITAIFA NA KAZI ZAO

90. Kutakuwa na Viongozi Wakuu Kitaifa wa Chama wafuatao:-

Viongozi wakuu wa Chama wa Taifa

(a) Mwenyekiti wa Taifa
(b) Makamu Mwenyekiti
(c) Katibu Mkuu

91. (1) Mwenyekiti wa Taifa atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Mwenyekiti wa Chama wa Taifa na kazi zake

(a) Ndiye atakayekuwa Kiongozi Mkuu wa shughuli za Chama Kitaifa.

(b) Atakuwa msemaji Mkuu wa Chama kwa mujibu wa Katiba hii na maelekezo ya Mkutano Mkuu wa Taifa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(c) Ataongoza vikao vyote vya Mkutano Mkuu wa Taifa, vya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na vya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa ya Chama.

(d) Atakuwa na kura ya uamuzi endapo katika kikao anachokiongoza kura za wajumbe zitafungana.

(e) Atajenga uhusiano mzuri na viongozi wa Kitaifa wa vyama vingine vya siasa ndani na nje ya nchi.

(f) Atateua kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, au wanachama wajasiri wa Chama, Wakurugenzi na Manaibu wakurugenzi wa Kurugenzi za Chama Kitaifa, Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa na Naibu Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.
Ila ijulikane kuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na wanachama wajasiri wa Chama walioteuliwa kuwa Wakurugenzi/Manaibu Wakurugenzi, Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na Naibu Katibu wa Ulinzi na Usalama ambao hawakuwa wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kabla ya kuteuliwa kushika nyadhifa hizo watasita kuwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa mara tu baada ya kusita kushika nyadhifa hizo.

(g) Atateua wanachama kumi na watano (15); ambapo tisa (09) kutoka Tanzania Bara, angalau watatu (03) wakiwa ni wanawake na sita (06) kutoka Zanzibar, angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake, kuwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kuthibitishwa.

(h) Atateua wanachama walemavu watano (05), watatu (03) kutoka Tanzania Bara, na wawili (02) kutoka Zanzibar kuwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kuthibitishwa.

(i) Atateua wanachama kumi (10); ambapo sita (6) kutoka Tanzania Bara, angalau wawili (2) wakiwa ni wanawake, na wanne (4) kutoka Zanzibar, angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake kuwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na wanachama wajasiri wa Chama na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

(j) Atateua wanachama walemavu wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar kuwa Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa au wanachama wajasiri wa Chama, na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa. Ila ifahamike mjumbe mmoja atakuwa mwanamke na mwengine atakuwa mwanamme.

(k) Atateua wanachama wanne (4);ambapo wawili (2), angalau mmoja akiwa mwanamke kutoka Tanzania Bara na wawili (2), angalau mmoja akiwa mwanamke kutoka Zanzibar, kuwa wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, na wanachama wajasiri wa Chama na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

(l) Atateua Makatibu Watendaji na Manaibu Katibu Watendaji wa Jumuiya zote za Chama baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mabaraza ya Taifa ya Jumuiya hizo, na kufikisha uteuzi wake huo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

(m) Atapendekeza kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, majina yasiyozidi manne (04), mawili (02) kutoka Tanzania Bara na mawili (02) kutoka Zanzibar ya watu wenye sifa za kuwa Naibu Katibu Mkuu na kuyawasilisha majina manne (04) hayo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kupigiwa kura ili wachaguliwe Manaibu Katibu Mkuu wawili (02), mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar.

(2) Endapo Mwenyekiti wa Chama wa Taifa atatokea upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu watatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.

92. (1) Kutakuwa na Makamu Mwenyekiti wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Makamu Mwenyekiti na kazi zake

(a) Atakuwa Msaidizi na Mshauri Mkuu wa Mwenyekiti wa Taifa.

(b) Atakuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama ya Taifa.

(c) Atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Chama.

(d) Atakuwa Mlezi Mkuu wa Jumuiya zote za Chama

(e) Atajenga uhusiano wa karibu sana wenye uelewano na Viongozi wa Kitaifa wa vyama vingine vya siasa ndani na nje ya nchi.

(f) Ataongoza vikao vya Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama ya Taifa pale Mwenyekiti wa Taifa atakaposhindwa kuhudhuria kikao chochote.

(2) Makamu Mwenyekiti pia atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au Mwenyekiti wa Taifa.

93. (1) Kutakuwa na Katibu Mkuu wa Chama ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Katibu Mkuu wa Chama na kazi zake

(a) Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Chama na pia mwajibikaji mkuu wa shughuli zote za utendaji za Chama Kitaifa.

(b) Atafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Mwenyekiti wa Taifa na Makamu Mwenyekiti.

(c) Atakuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Chama ya Taifa.

(d) Atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Utendaji ya Taifa ya Chama.

(e) Atajenga mahusiano mema na Makatibu Wakuu wa vyama vingine vya siasa nchini na nje ya nchi.

(f) Atakuwa dhamana wa ofisi za Makao Makuu na Ofisi Kuu ya Chama.

(g) Atahakikisha kwamba nyaraka zote za Chama nchini zinatunzwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

(h) Atahakikisha kuwepo na kuhifadhiwa kwa kumbukumbu za vikao vyote vya Chama vya Taifa.

(i) Atakuwa mwajibikaji mkuu wa mambo yote ya fedha na mali za Chama katika ngazi ya Taifa (Chief Accounting Officer).

(j) Atatayarisha na kuhifadhi taarifa binafsi za Viongozi Wakuu wa Chama na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Viongozi wa Serikali watokanao na Chama.

(k) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Mwenyekiti wa Taifa na Makamu Mwenyekiti.

(2) Katibu Mkuu atakuwa ndiye katibu wa vikao vya Mkutano Mkuu wa Taifa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(3) Katibu Mkuu atapokuwa nje ya nchi au atakaposhindwa kufanya kazi zake kwa sababu yoyote ile, Naibu Katibu Mkuu anayemfuata kwa madaraka atakuwa Kaimu Katibu Mkuu hadi pale Katibu Mkuu atapokuwa tayari kuendelea kutekeleza majukumu yake.

94. (1) Viongozi Wakuu wa Chama, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu wanaweza kusimamishwa uongozi na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 83 (1) cha Katiba hii.

Kusimamishwa/ kufukuzwa uongozi Viongozi Wakuu wa Chama wa Taifa

(2) Baada ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kumsimamisha uongozi Kiongozi Mkuu yeyote wa Chama, litawasilisha taarifa kamili ya sababu za kumsimamisha uongozi Kiongozi Mkuu huyo kwa Mkutano Mkuu wa Taifa katika muda usiozidi siku tisini (90) tangu uamuzi huo utolewe.

(3) Mkutano Mkuu wa Taifa ndio pekee wenye uwezo wa kumuachisha au kumfukuza uongozi Kiongozi Mkuu wa Chama kwa kufuata masharti ya Katiba hii, na uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(4) Endapo Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Katibu Mkuu watasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi, mwanachama wa kukaimu nafasi atapatikana kwa mujibu wa masharti ya vijifungu vya 105 (1) na (3) vya Katiba hii.

(5) Endapo Kiongozi Mkuu wa Chama ataachishwa au kufukuzwa uongozi basi uchaguzi wa kujaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kuvuliwa madaraka Kiongozi Mkuu yeyote utaitishwa katika kipindi kisichopungua siku mia moja na themanini (180) tangu nafasi hiyo iwe wazi.

95. (1) Kutakuwa na Manaibu Katibu Mkuu wawili (02) wenye mamlaka sawa kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano watakaochaguliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa mujibu wa mapendekezo ya Mwenyekiti wa Taifa.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama

(2) Naibu Katibu Mkuu mmoja atakuwa Mshauri na Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu kwa upande wa Tanzania Bara, na mwengine atakuwa Mshauri na Msaidizi Mkuu wa Katibu Mkuu kwa upande wa Zanzibar, ingawa upeo wa madaraka ya kila Naibu Katibu Mkuu utakuwa kwa Tanzania nzima kwa wakati wote wa utendaji wa shughuli za Chama.

(3) Naibu Katibu Mkuu atakayemfuatia Katibu Mkuu kwa madaraka ni yule anayetoka upande tofauti wa Jamhuri ya Muungano na upande anaotoka Katibu Mkuu.

96. Naibu Katibu Mkuu wa Chama atakuwa na majukumu yafuatayo:-

Kazi za Naibu Katibu Mkuu

(1) Kusimamia shughuli, taratibu na Kanuni za utawala za Chama za kila siku katika eneo lake la kazi.

(2) Atakuwa Katibu wa vikao vya Kamati ya Utendaji ya Taifa pale kikao hicho kitapofanyika katika eneo lake la kazi.

(3) Atasimamia uandishi na utunzaji wa mihitasari yote ya vikao vya Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(4) Atasimamia na kuratibu utekelezaji wa sera na ilani ya uchaguzi unaofanywa na serikali inayoongozwa na CUF au mawaziri kutoka Chama.

(5) Atahakikisha kufanyika kwa vikao vya mashauriano vya kila wiki vinavyowashirikisha Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi waliopo katika eneo lake la kazi na kuviongoza vikao hivyo pale Katibu Mkuu asipokuwepo.

(6) Atahakikisha kuwepo kwa usimamizi wa karibu wa halmashauri za wilaya, mabaraza ya miji, serikali za mitaa, vijiji na vitongoji zinazoongozwa na Chama katika eneo lake la kazi.

(7) Atafanya kazi nyingine zozote atakazopewa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu.

Kusimamishwa/ kufukuzwa uongozi Naibu Katibu Mkuu

97. (1) Naibu Katibu Mkuu anaweza kusimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi na, au uanachama na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(2) Naibu Katibu Mkuu aliyesimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi au uanachama ana haki ya kukata Rufaa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa ambao uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

(3) Endapo Naibu Katibu Mkuu atasimamishwa, kuachishwa au kufukuzwa uongozi, mwanachama wa kukaimu nafasi hiyo atapatikana kwa mujibu wa masharti ya vijifungu (1) na (3) vya Kifungu cha 105 cha Katiba hii.

(4) Endapo Naibu Katibu Mkuu ataachishwa au kufukuzwa uongozi, basi Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litachagua mwanachama mwingine kujaza nafasi hiyo kwa mujibu wa mashairi ya Katiba hii.

SURA YA NNE

BODI YA WADHAMINI, KAMATI, TAASISI NA KURUGENZI ZA CHAMA.

98. (1) Kutakuwa na Bodi ya Wadhamini ya Chama itakayoteuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa mujibu wa sheria za nchi kwa kipindi cha miaka mitano (05) na mjumbe anaweza kuteuliwa tena baada ya muda wake kumalizika.

Bodi ya Wadhamini

(2) Bodi itakuwa na wajumbe wasiozidi tisa (09), watano (05) kutoka Bara angalau wawili (02) wakiwa ni wanawake na wane (04) kutoka Zanzibar angalau mmoja (01) akiwa ni mwanamke ambao watateuliwa kwa masharti yanayohitajika ya sheria ya Bodi ya Wadhamini na utaratibu uliowekwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(3) Bodi ya Wadhamini itakuwa ndiyo mdhamini pekee wa fedha na mali za Chama pamoja na madeni na itafanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa na sheria ya nchi inayohusu Wadhamini.

(4) Bodi inaweza kushitaki au kushitakiwa kwa niaba ya Chama.

(5) Bodi itawajibika kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa la Chama ambalo linaweza kuweka utaratibu unaofaa wa kuendesha shughuli za Bodi hiyo, na itafanya vikao vyake angalau mara mbili kwa mwaka.

(6) Mwenyekiti na Naibu Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini watachaguliwa na Wajumbe wa Bodi kutoka miongoni mwao, kwa sharti kwamba Mwenyekiti akitoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Naibu Mwenyekiti atatoka upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano.

99. (1) Kutakuwa na Kamati ya Maadili na Nidhamu itayowajibika kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa ambayo itafanya vikao vyake kila pale itapohitajika, lakini sio chini ya mara moja kila baada ya miezi sita.

Kamati ya Maadili na Nidhamu

(2) Wajumbe wa Kamati ya Maadili na Nidhamu watakuwa ni:-

Wajumbe wa Kamati ya Maadili na Nidhamu

(i) Makamu Mwenyekiti wa Chama
(ii) Manaibu Katibu Mkuu
(iii) Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama
(iv) Naibu Mkurugenzi wa Ulinzi na Usalama
(vi) Wajumbe wengine watatu akiwemo angalau mwanamke mmoja na mwanasheria mmoja na angalau mmoja kutoka Zanzibar, watakaoteuliwa na Mwenyekiti wa Taifa baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au wanachama wajasiri wa Chama.

100. Majukumu ya Kamati ya Maadili na Nidhamu yaakuwa kama ifuaravyo:-

Majukumu ya Kamati ya Maadili na Nidhamu

(1) Kufuatilia nyendo za wanachama na viongozi wa Chama ili kuhakikisha kuwa kila mmoja miongoni mwao anatunza maadili mema ya Chama na maadili ya uongozi.

(2) Kuhakikisha kuwa wanachama na viongozi wanakuwa na nidhamu ndani ya Chama na nje ya Chama ili kukijengea taswira njema Chama katika umma.

(3) Kufanya uchunguzi juu ya taarifa za uvunjifu wa maadili na nidhamu yanayotolewa dhidi ya mwanachama, kiongozi, au kikao cha Chama, na kuchukua hatua kwa mujibu wa masharti ya katiba hii au kanuni zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(4) Kufanya jambo jingine lolote lile ambalo Kamati itaagizwa kulifanya na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, au ambalo Kamati yenyewe wataliona linafaa kufanywa kwa madhumuni ya kukilinda na kukinusuru Chama.

101. (1) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza, pindi likiona inafaa, kuanzisha Kamati, Tume au Taasisi yoyote ile ya Kitaifa yenye lengo la kusaidia utekelezaji mzuri wa sera na itikadi za Chama, au kufanya uchunguzi juu ya jambo lolote lile linalohitaji kufanyiwa uchunguzi.

Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuanzisha Kamati/Taasisi za Kitaifa

(2) Pale ambapo Baraza Kuu la Uongozi la Taifa limeanzisha Kamati, Tume au Taasisi yoyote ya Kitaifa basi pia litatoa maelekezo ya namna ya wajumbe wake watakavyopatikana pamoja na hadidu za rejea za chombo hicho.

102. (1) Katika utekelezaji wa shughuli zake chini ya Kifungu 82 cha Katiba hii au shughuli nyingine yeyote iliyopewa na Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuanzisha kurugenzi ya aina yoyote ile ya ngazi ya Taifa na Kitengo cho chote cha ngazi ya wilaya katika kusaidia utekelezaji mzuri wa shughuli za Chama.

Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kuanzisha Kurugenzi

(2) Kila Kurugenzi itaongozwa na Mkurugenzi akisaidiwa na Naibu Mkurugenzi atakayetoka upande tofauti wa Jamhuri ya Muungano ambao Mkurugenzi wake anatoka.

(3) Kila Kitengo katika wilaya kitaongozwa na Mkuu wa Kitengo atakayeteuliwa na Mwenyekiti wa wilaya baada ya Kushauriana na Katibu wa wilaya na kisha kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa wilaya, kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa wilaya.

(4) Mwenyekiti wa Taifa kwa kushauriana na Makamu Mwenyekiti ndiye atakayeteua Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi na baadae kufikisha uteuzi wake kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

(5) Majukumu ya kila Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi wa ngazi ya Taifa, na majukumu ya kila Mkuu wa Kitengo cha Chama kwa ngazi ya wilaya zitaelezewa mara kwa mara katika Kanuni za Kurugenzi na Vitengo hivyo zitazotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

103. (1) Kutakuwa na Jumuiya za Chama zifuatazo ambazo zitafanya shughuli zao kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa:

Jumuiya za Chama

(a) Jumuiya ya Wanawake (JUKECUF)
(b) Jumuiya ya Vijana (JUVICUF)
(c) Jumuiya ya Wazee (JUZECUF)

(2) Kila Jumuiya ya Chama itakuwa na

(a) Mwenyekiti wa Jumuiya wa Taifa atakayekuwa kiongozi Mkuu na msemaji Mkuu wa Jumuiya ambaye atachaguliwa na Mkuatno Mkuu wa Taifa wa Jumuiya.

(b) Makamo Mwenyekiti ambaye atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Jumuiya kwa masharti kwamba Mwenyekiti akitoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atoke upande mwengine wa Jamhuri ya Muungano.

(c) Katibu Mtendaji wa Jumuiya ambaye atakuwa ndio Mtendaji mkuu wa Jumuiya ambaye atateuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Taifa la Jumuiya husika na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa. Katibu Mtendaji wa Jumuiya atatoka upande tafauti wa Jmhuri ya Muungano na upande anaotoka Mwenyekiti wa Taifa wa Jumuiya.

(d) Naibu Katibu Mtendaji wa Jumuiya atateuliwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Taifa la Jumuiya husika na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, kwa masharti kwamba atatoka upande wa Jamhuri ya Muungano tafauti na ule anakotoka Katibu Mtendaji.

(3) Vikao vya kitaifa na vya ngazi nyengine vitakuwa kama vitakavyowekwa katika Kanuni za Jumuiya.

(4) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza, likihisi inafaa na ni kwa maslahi ya Chama, kuelekeza, kuthibitisha na/au kubatilisha maamuzi yoyote yale yaliyofanywa na Jumuiya katika ngazi yoyote ile.

(5) Kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Jumuiya na kwa ajili ya kuwa na utaratibu mzuri wa shughuli za Chama, na bila kuathiri masharti ya kijifungu cha (3) cha Kifungu hiki pamoja na masharti ya Kifungu cha 13 cha Katiba hii,kila Jumuiya katika ngazi husika itawajibika kwa Chama katika ngazi hiyo.

SURA YA TANO

TARATIBU ZA UCHAGUZI KATIKA CHAMA

Uchaguzi wa viongozi wa Chama

104. (1) Mgombea yeyote yule anaetaka kugombea nafasi yoyote ile ya Chama au ya serikali kwa kupitia tiketi ya Chama katika ngazi ya Tawi, Kata Jimbo, wilaya au Taifa atafuata utaratibu chini ya kanuni zitakazotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa na kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa ajili hiyo.

(2) Kamati ya Utendaji ya Taifa inapohisi inafaa itatunga kanuni za Uchaguzi mara kwa mara kwa ajili ya chaguzi zilizoelezewa chini ya kijifungu cha (1) cha Kifungu hiki au chaguzi nyengine zozote zinazoweza kutokea ndani ya Chama katika ngazi yeyote ile na kisha kuzifikisha kanuni hizo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

(3) Hakuna Kanuni ya Uchaguzi zitakazotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa juu ya mambo yanayohusiana na uchaguzi zitakazoanza kutumika bila ya kwanza kuthibitishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

(4) Uchaguzi Mkuu wa Chama utafanyika kila baada ya miaka mitano, lakini chaguzi nyingine ndogo ndogo zinaweza kufanyika wakati wowote ule ambapo Baraza Kuu la Uongozi la Taifa au Kamati ya Utendaji ya Taifa itaelekeza kutokana na kujitokeza haja ya kufanya uchaguzi huo kwa sababu za dharura zinazoweza kujitokeza mara kwa mara.

SURA YA SITA

MENGINEYO

Kukaimu madaraka

105. (1) Pale ambapo mwanachama yeyote wa Chama mwenye madaraka kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kwa sababu yoyote ile, hawezi kutekeleza kazi zake kwa muda, au amesimamishwa au kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, mamlaka iliyo na uwezo wa uchaguzi au uteuzi wa nafasi hiyo inaweza kumteua mwanachama mwingine mwenye sifa zinazohitajika kukaimu madaraka hayo.

(2) Pale ambapo nafasi ya Katibu wa wilaya iko wazi kwa sababu yeyote ile, Mkuu wa Kitengo kinachohusiana na Mipango na Uchaguzi ndiye atakaye kaimu nafasi ya Katibu wa wilaya.

(3) Kukaimu kwa madaraka hayo kutasita mara tu baada ya mtu aliyekaimiwa atakaporudi katika nafasi yake au mwanachama mwingine kuchaguliwa au kuteuliwa kujaza nafasi hiyo, na kwa vyovyote vile kukaimu huko hakutozidi vipindi viwili vya miezi sita kwa kila kipindi bila ya nafasi hiyo kujazwa kwa mujibu kwa masharti ya Katiba hii.

Ofisi zilizoanzishwa

106. Ofisi yoyote maalum itakayoanzishwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa itasimamiwa na Ofisa Mtendaji mwenye ujuzi wa kutosha kusimamia kazi za ofisi hiyo lakini italazimu Baraza Kuu la Uongozi la Taifa lipeleke taarifa ya kuanzishwa kwa Ofisi hiyo katika kikao kinachofuata cha Mkutano Mkuu wa Taifa.

Fedha za Chama

107. (1) Chama kinaweza kupata mfuko wake wa fedha kutokana na moja au zaidi ya mambo haya yanayofuata:-

(i) Ada za wanachama.

(ii) Ruzuku kutoka serikalini.

(iii) Michango ya Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na viongozi wengine wa serikali kutoka Chama ambao Baraza Kuu litaamua wawe wanakichangia Chama.

(iv) Mikopo, ruzuku au misaada kutoka Chama, chombo, taasisi, mtu binafsi au pahala pengine popote ndani au nje ya nchi, mradi sheria za nchi hazitakiukwa.

(v) Mapato kutokana na miradi ya uchumi, biashara, tafrija, michango au shughuli yoyote ile ya kihalali ama ya ndani au ya nje ya nchi.

(vi) Chanzo kingine chochote kile ambacho Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litaidhinisha.

(2) Malipo yote kwa Chama ngazi ya Taifa yatawasilishwa katika Ofisi ya Katibu Mkuu, na kwa ngazi nyingine za Chama malipo hayo yatawasilishwa katika ofisi za makatibu wa Chama wa ngazi hizo.

(3) Kamati ya Utendaji ya Taifa inaweza kutunga Kanuni juu ya upatikanaji na utozwaji wa fedha kwa wanachama kwa njia ya mchango au vinginevyo pamoja na kubuni na kusimamia miradi ya uzalishaji ya Chama, na Kanuni za udhibiti na matumizi ya fedha na kisha kufikisha kanuni hizo mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kuthibitishwa.

Nidhamu ya Chama na muda wa kukata Rufaa

108. (1) Bila ya kuathiri masharti ya vifungu vyingine vya Katiba hii Kamati ya Utendaji ya kila ngazi itashughulikia nidhamu na baadaye kupeleka mapendekezo yake kwa Mkutano Mkuu wa ngazi inayohusika. Kwa ngazi ya Taifa mapendekezo ya Kamati ya Utendaji ya Taifa yatafikishwa mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, kabla ya kufikishwa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa pale itapobidi kufanya hivyo.

(2) Kamati ya Utendaji ya Taifa, baada ya kujiridhisha kuwa kuna haja ya kukiokoa Chama, kutokana na matatizo yaliyopo katika ngazi yo yote ya chini, kuanzia ngazi ya wilaya hadi ngazi ya Tawi ya Chama, inaweza kuuvunja au kuusimamisha uongozi wa ngazi hiyo ya chini na kuweka uongozi wa muda, na baadae, kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kuweka uongozi wa kudumu au kuelekeza vyenginevyo.

(3) Maamuzi ya Kamati ya Utendaji ya Taifa kuhusu jambo hili yatafikishwa mbele ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa taarifa.

(4) Hatua za kinidhamu katika Chama ni pamoja na onyo, onyo kali, onyo la maandishi, karipio, karipio kali, kusimamishwa, kuachishwa nafasi ya uongozi, kufukuzwa uongozi, pamoja na kufukuzwa uanachama, ila tu ijulikane kuwa si lazima kwa chombo kinachohusika kuchukua hatua hizo za nidhamu kwa mpangilio huo, bali kinaweza kuchukua hatua yoyote ile au zaidi ya hatua moja kwa pamoja kutegemeana na uzito wa kosa lililofanywa.

(5) Mwanachama au kiongozi yeyote aliyeamua kukata Rufaa kwa jambo lolote lile, basi atafanya hivyo kwa ngazi iliyo juu ya kikao kilichotoa maamuzi ambayo hakuridhika nayo katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne (14) tokea siku uliotolewa uamuzi huo.

109. Chama kitakuwa mstari wa mbele katika kuelimisha na kuwafanya wanachama wake:-

Chama kuelimisha wanachama wake

(1) Kujua na kuelewa elimu ya uraia mwema na nidhamu ya kazi.

(2) Kuheshimu na kukosoa mawazo ya wengine kwa misingi ya ukweli, na heshima , kwa minajili ya kuweka nidhamu nzuri katika Chama.

(3) Kuelewa haki yake ya kusikilizwa, kujitetea na kukata rufaa juu ya maamuzi yoyote yaliyochukuliwa dhidi yake.

(4) Kutetea na kutekeleza usawa na haki mbele ya sheria kwa lengo la kuleta maelewano na utendaji wa kinidhamu katika Chama.

Kanuni za Chama

110. (1) Bila ya kuathiri Kifungu kingine chochote katika Katiba hii Kamati ya Utendaji ya Taifa inaweza kutunga Kanuni za Chama kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa sera na malengo ya Chama kwa kuzingatia misingi ya Katiba hii.

(2) Kanuni zote zilizotungwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa itabidi ziidhinishwe na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Lugha rasmi ya Chama

111. Chama kitawasiliana katika shughuli zake zote za ndani na nje ya nchi kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kiingereza kwa kadiri itakavyohitajika.

Kukasimu madaraka

112 (1) Madaraka, uwezo na nguvu za Chama zinaweza kukasimiwa kutoka kikao cha juu kwenda kikao cha chini kama ifuatavyo:-

a) Mkutano Mkuu wa Taifa unaweza kukakasimu madaraka yake kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

b) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kukasimu madara kwa Kamati ya Utendaji ya Taifa. Ila ijulikane tu kwamba majukumu yale yanayohusu kuchagua, kuteua, kusimamisha, kuachisha au kufukuza viongozi au mwanachama hayawezi kukasimiwa kwa chombo kingine chochote, Isipokuwa kwa utaratibu ulioelezwa chini ya kijifungu kidogo cha (c) cha Kifungu hiki.

c) Iwapo itatokea ulazima wa kuwepo uchaguzi mdogo wa ubunge au uwakilishi, au iwapo mgombea aliyeteuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa atashindwa kuendelea kuwa mgombea kwa sababu yoyote ile ;na kwamba ni vigumu kuitishwa kwa wakati huo Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa ajili ya uteuzi mwingine, Kamati Utendaji ya Taifa itamteua mgombea mwingine wa kujaza nafasi hiyo kwa utaratibu ule ule uliowekwa chini ya kifungu cha 104(1) na

(2) cha Katiba hii au ikiwa haiwezekani Kamati ya Utendaji ya Taifa itaweka utarabu wake wa kumpata mgombea mwingine na maamuzi yake yatakuwa ya mwisho. Maamuzi hayo yatapelekwa kwenye kikao cha Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kinachofuata kwa taarifa yake.

d) Ngazi yoyote ya juu ya chama inaweza kukasimu madaraka yake kwa ngazi yoyote iliyoko chini yake kama itaonekana na ngazi hiyo kwamba inafaa kufanya hivyo.

(2) Iwapo itatokea kuwa na uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano au Rais wa Zanzabar ghafla, au pale ambapo mgombea wa nafasi hiyo hawezi kuendelea na kampeini zake baada ya kuteuliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa chini ya kifungu 79(1p) kwa sababu ya:-

(i) Kufariki dunia au
(ii) Ugonjwa au
(iii) Kujiuzulu au
(iv) Sababu nyingine yoyote ile,

ambayo itamfanya mgombea huyo kutoendelea na nafasi hiyo, na ikiwa ni vigumu kwa wakati huo kuitisha Mkutano Mkuu wa Taifa kwa ajili ya uteuzi mwingine, Baraza Kuu la Uongozi la Taifa litafanya uteuzi wa mwanachama mwingine mwenye sifa kuwa mgombea wa nafasi iliyoachwa wazi na kisha kupeleka taarifa ya uteuzi huo kwa Mkutano Mkuu wa Taifa unaofuata. Mwanachama huyo aliyeteuliwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa atakuwa ni mgombea halali wa Chama wa nafasi hiyo iliyoachwa wazi.

(3) Ikiwa litatokea jambo lolote lile kwa mgombea mwenza kama yale yaliyoelezwa chini ya kijifungu kidogo cha (2) kwa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano au Urais wa Zanzibar, na kwamba ni vigumu kuitisha Baraza Kuu la Uongozi la Taifa kwa kipindi hicho, mgombea wa kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atafikisha mbele ya Kamati ya Utendaji ya Taifa jina la mwanachama mwenye sifa na ambaye anampendekeza kuwa mgombea mwenza ili athibitishwe na baadae Kamati ya Utendaji ya Taifa itapeleka taarifa ya shughuli hiyo kwa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa katika kikao kinachofuata.

(4) Iwapo itatokezea kuwa na uchaguzi wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano au Rais wa Zanzibar kwa ghafla na kwamba hali na muda haviruhusu kuitishwa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa basi kifungu hiki kitatumika kwa kukasimu madaraka ya Mkutano Mkuu chini ya kifungu 79(1p) kwa kuliidhinisha Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, kupiga kura za siri na kufanya shughuli hiyo ya uteuzi wa mgombea Urais na baadaye kupeleka taarifa ya shughuli hiyo kwa Mkutano Mkuu wa Taifa unaofuata.

(5) Pale ambapo kuna haja ya kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura wa ngazi husika isiyokuwa ngazi ya Taifa, na kwamba Kamati ya Utendaji ya ngazi hiyo, kwa sababu moja au nyingine, haikuweza au haitaki kuitisha Mkutano Mkuu huo wa dharura, basi wajumbe wa Mkutano Mkuu huo wasiopungua theluthi mbili (2/3) ya idadi yao wataweza kutoa azimio ambalo litatiwa saini na wajumbe hao wote la kutaka Mkutano Mkuu uitishwe na kisha kukabidhi azimio hilo kwa katibu wa Kamati ya Utendaji ya ngazi hiyo.

(6) Kamati ya utendaji ya ngazi husika italazimika kuitisha Mkutano Mkuu wa dharura wa ngazi hiyo katika kipindi kisichozidi siku tisini (90) tangu azimio la wajumbe wa Mkutano Mkuu huo kuwasilishwa na kupokelewa na katibu wa Kamati ya Utendaji hiyo.

113. Isipokuwa pale ambapo Katiba imeeleza vinginevyo masharti ya kuchaguliwa kwa kiongozi na kipindi cha uongozi kitakuwa kama hivi:-

Masharti ya kuchaguliwa na kipindi cha uongozi

(1) Kipindi cha uongozi wa Chama kitakuwa miaka mitano (5) kwa ngazi zote isipokuwa kama kiongozi huyo ameshindwa kazi aliyopewa.

(2) Iwapo kipindi cha uongozi kimemalizika na kuna sababu za msingi na za Kitaifa kusababisha kwamba uchaguzi wa viongozi hao hauwezi kufanyika basi muda wa uongozi utaendelea kwa kipindi kingine cha miezi isiyozidi sita (06) na baada ya hapo ni lazima uchaguzi mpya uitishwe.

(3) Mwanachama wa Chama hiki atakuwa na fursa sawa na mwanachama mwingine yeyote ya kuchagua na au kuchaguliwa kushika nafasi ya uongozi katika Chama na serikali kupitia Chama katika ngazi yoyote ile, ila tu pale ambapo mwanachama amefukuzwa au kuachishwa uongozi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, basi hatoweza kuchaguliwa tena hadi kipindi cha miaka miwili (02) kuanzia siku aliyofukuzwa au kuachishwa uongozi kimalizike.

(4) Kiongozi anaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano (5) baada ya muda wake kumalizika, na anaweza kuchaguliwa hivyo kwa muda wote ambao wanachama watamkubali.

(5) Mgombea uchaguzi wowote wa Kitaifa wa Chama sharti awe na umri usiopungua miaka ishirini na moja (21) na anayejua kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza. Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu na mgombea nafasi ya Urais wa Jamuhuri ya Muungano na Urais wa Zanzibar lazima awe na umri usiopungua miaka 35 isipokuwa pale sheria za nchi zimeagiza vinginevyo.

(6) Mwanachama mpya wa Chama hataweza kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya uongozi katika Chama kwa ngazi yoyote ile hadi hapo mwanachama huyo ametimiza angalau miezi sita (06) kama mwanachama, isipokuwa pale ambapo pameanzishwa Tawi jipya na ambapo wanachama wa Tawi hilo wote ni wapya. Katika mazingira hayo masharti ya kijifungu hiki hayatatumika, ila viongozi wa muda wa Tawi watachaguliwa na watashika madaraka kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi tisa (9) ambapo itabidi viongozi wa kudumu wa Tawi wachaguliwe.

(7) Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kuyaweka upande masharti ya kijifungu cha (6) cha Kifungu hiki na kuruhusu kuchaguliwa au kuteuliwa kwa mwanachama yeyote yule asiyetimiza umri wa miezi sita kama mwanachama ikiwa, kwa kufanya hivyo ni kwa maslahi ya Chama alimradi tu mwanachama huyo awe anatimiza sifa nyingine za kuchaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Kuhalalisha kikao

114. Isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Katiba hii, kiwango cha wajumbe cha kuhalalisha kikao chochote cha Chama ni zaidi ya nusu ya wajumbe wote wa kikao hicho.

115. Ila pale ambapo imeelezewa vinginevyo katika Katiba hii:-

Uhalali wa Maamuzi

(1) Uamuzi wowote ule utafikiwa kwa kura za wajumbe ambazo zinapita nusu ya wajumbe waliohudhuria katika kikao hicho.

(2) Kijifungu cha (1) cha Kifungu hiki hakitoathiri uamuzi unaofikiwa kwa muafaka

(3) Katika shughuli za uchaguzi wowote ule kura zitakuwa za siri.

(4) Masharti ya kifungu hiki hayotoathiri masharti ya vifungu vingine vyovyote vya Katiba hii ambavyo vimetoa masharti ya upigaji kura juu ya suala lolote.

Mialiko kwa Wataalamu

116. Kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote ile kitakuwa na uwezo wa kuwakaribisha watu wasiokuwa wajumbe wa kikao hicho, ikiwa ni pamoja na wataalamu, kwa madhumuni ya kuwasikiliza au kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu au ushauri mwingine. Ifahamike kwamba watu waliokaribishwa hawatakuwa na haki ya kushiriki katika kutoa maamuzi au kupiga kura.

117. (1) Kiongozi yeyote wa chama anaweza kujiuzulu uongozi wake wakati wowote ule.

Kujiuzulu uongozi

(2) Kiongozi atajiuzulu kwa kuandika barua na kuweka saini yake kwa katibu wa mamlaka iliyomchagua au kumteua na kiongozi huyo atahesabiwa kuwa amejiuzulu ikifika tarehe aliyoainisha katika barua yake kuwa atajiuzulu pindipo akikubaliwa

na mamlaka iliyomchagua au iliyomteua, au kama hakuainisha tarehe ya kujiuzulu kwake basi atahesabiwa amejiuzulu mara baada ya katibu wa mamlaka iliyomteua au kumchagua kupokea barua hiyo na mamlaka iliyomchagua au kumteua kukubali.

Uwezo wa kuunda Kamati za muda

118. Kikao chochote cha Chama katika ngazi yoyote ile kinaweza, haja ikitokea, kuunda Kamati na/au Tume ya muda kwa ajili ya kuchunguza jambo au kufanya shughuli yeyote itakayoelekezwa kufanywa na kikao chenyewe. Kamati na/au Tume iliyoundwa ni lazima kupewa majukumu yaliyo wazi na kupewa muda wa kukamilisha kazi yake. Uhalali wa Kamati na/au Tume ya muda utakwisha pale inapowasilisha taarifa yake na kupokelewa na kikao kilichounda Kamati na/au Tume hiyo ya muda, isipokuwa muda wa Kamati au Tume ya muda unaweza kuongezwa na kikao kilichounda tume hiyo ya muda.

Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wa CUF

119. (1) Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walioingia katika Bunge hilo kwa tiketi ya Chama hiki kwa pamoja wataunda kundi la wabunge wa "The Civic United Front (CUF – Chama Cha Wananchi)" katika Bunge hilo.

(2) Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar walioingia katika Baraza la Wawakilishi kwa tiketi ya Chama hiki kwa pamoja wataunda kundi la Wawakilishi wa "The Civic United Front – (CUF – Chama cha Wananchi)'' katika Baraza hilo.

(3) Madiwani wote waliochaguliwa kwa tiketi ya Chama wataunda kundi la madiwani wa CUF ambapo wanaweza kukutana mara kwa mara au inapotokea haja ya lazima kwa kujadili masuala muhimu ya Chama katika Kata au Wodi zao, au mambo mengine ambayo Chama kwa kupitia ngazi zake za Chama kitaelekeza, ila ijulikane tu kuwa shughuli zao zote zitazingatia pia uwezo, madaraka na nguvu walizopewa na sheria za nchi zinazoanzisha madiwani.

120. Kila kiongozi wa serikali kwa tiketi ya Chama atalazimika :-

Wajibu wa kiongozi wa serikali kwa tiketi ya Chama

(1) Kukichangia Chama

(2) Kushiriki katika shughuli zote za Chama

(3) Kutunza maadili na taratibu za Chama

(4) Kutoa taarifa za utendaji wa shughuli zake za kikazi mbele ya Kamati ya Utendaji ya ngazi yake inayomhusu na

(5) Kufanya jingine lolote atakaloagizwa na Chama, kuwa afanye kwa utaratibu maalum utakaowekwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, na kwamba pale ambapo kiongozi huyo hatatekeleza moja au zaidi ya moja ya mambo hayo yaliyoelezwa katika

kifungu hiki, basi Baraza Kuu la Uongozi la Taifa linaweza kumchukulia hatua yoyote ya kinidhamu ikiwemo ya kuachishwa au kufukuzwa uongozi na/au uanachama wake kwa mujibu wa matakwa ya Katiba hii.

121. (1) Kundi la Wabunge na/au la Wawakilishi wa Chama litaongozwa na kiongozi atakayepatikana kwa mujibu wa taratibu za Bunge na za Baraza la Wawakilishi na taratibu zilizowekwa na Baraza Kuu la Uongozi la Taifa

(2) Kundi la Wabunge au la Wawakilishi wa Chama linaweza kutunga Kanuni na taratibu zake ambazo Wabunge au Wawakilishi hao watahisi zinafaa kwa uendeshaji mzuri wa shughuli zao katika Bunge au katika Baraza la Wawakilishi.

Wabunge/ Wawakilishi kutunga Kanuni

122. (1) Mjumbe wa kikao ni lazima ahudhurie mikutano yote ambayo yeye ni mjumbe na pale ambapo hatohudhuria kwa sababu maalum itambidi amuarifu katibu wa kikao hicho kwa maandishi.

Mahudhurio ya kikao cha Chama

(2) Mjumbe anayekosa kuhudhuria vikao vitatu (3) mfululizo ambavyo anatakiwa ki-katiba ahudhurie bila ya sababu inayokubalika basi atasita kuwa mjumbe wa kikao hicho.

123. Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi wote wa Kurugenzi za Chama watakuwa na ofisi zao katika Makao Makuu ya Chama, na/au Ofisi Kuu ya Chama, lakini kiongozi yeyote aliyetajwa katika Kifungu hiki anaweza kufungua ofisi ya muda au kudumu katika sehemu nyingine ya nchi pindi akipata idhini ya Baraza Kuu la Uongozi la Taifa.

Ofisi za Viongozi wa Chama

124. Pale iwapo pana nafasi wazi ya mjumbe katika kikao chochote na cha ngazi yoyote ya Chama, mamlaka inayohusika itajaza nafasi hiyo kwa haraka, na kwa vyovyote si zaidi ya miezi sita (6) kwa kufuata utaratibu uliowekwa, na kwamba nafasi hiyo iliyowazi haitofanya kikao kinachohusika kisiendeshe mikutano yake ila tu pale ambapo Katiba hii inaelekeza vyenginevyo.

Kujaza nafasi zilizowazi

125. Katika Katiba hii maneno yafuatayo yatakuwa na maana iliyopewa mbele yake isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo:-

Tafsiri ya maneno mbali mbali

(a) "Chama" Maana yake ni "The CIVIC UNITED FRONT'' (CUF – Chama Cha Wananchi) na kwa kifupi "CUF"

(b) "Baraza Kuu la Uongozi la Taifa" ina maana ya Halmashauri Kuu ya Uongozi katika ngazi ya Kitaifa.

(c) "Haki za Binaadamu" ni haki ambazo mtu yeyote anakuwa nazo tangu kuzaliwa kwake, na ni kama zilivyotangazwa katika Tamko la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu.

(d) "Haki za Watu" ni haki za watu ambazo hutangazwa mara kwa mara na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, au Jumuiya nyinginezo zinazotambulika duniani.

(e) "Kamati ya Utendaji" ni sekretarieti ya Chama katika ngazi inayohusika ya Chama.

(f) "Katibu Mkuu" ina maanisha Katibu Mkuu wa Chama ambaye ndiye mtendaji Mkuu wa shughuli zote za Chama Kitaifa.

(g) "Kijana" inajumuisha kijana yeyote bila kujali jinsia ambaye atakubalika na Chama kuwa ni kijana, na kama itakavyoelezwa katika Kanuni za Chama.

(h) "Kitengo cha Chama" ina maana ya idara ya Chama katika ngazi ya wilaya.

(i) "Kukaimu madaraka" ina maana ya kumshikia kiongozi nafasi yake ya kazi mpaka hapo mwenye nafasi hiyo ataporejea kazini au hadi hapo nafasi hiyo itakapojazwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(j) "Kurugenzi ya Chama" ina maana ya Idara ya Chama katika ngazi ya Taifa.

(k) "Makamu Mwenyekiti" ina maana ya Msaidizi na Mshauri Mkuu wa Mwenyekiti Taifa.

(l) "Mwenyekiti wa Taifa" ina maana ya kiongozi Mkuu wa Chama Kitaifa na Msemaji Mkuu wa Chama ngazi ya Taifa.

(m) "Mkutano Mkuu" ina maana ya mamlaka ya juu kabisa ya Chama yenye maamuzi ya mwisho katika ngazi inayohusika ya Chama.

(n) "Mratibu wa Chama" ina maana ya kiungo cha Chama baina ya uongozi wa Tawi na wananchi wa eneo lenye mkusanyiko wa wananchi.

(o) "Mtumishi wa Chama" ina maana ya mwanachama aliyeteuliwa au kuchaguliwa kushika wadhifa wa uongozi au utendaji katika Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(p) "Mzee" ina maana ya mwanachama wa Chama aliyefikia umri wa miaka khamsini (50) au zaidi kwa mwanamke, au miaka khamsini na mitano (55) au zaidi kwa mwanamme.

(q) "Uliberali" ina maana ya itikadi ya mfumo wa kiuchumi, kisiasa, na kijamii wenye lengo la, kwa kadiri itakavyowezekana, kuleta haki sawa na neema kwa wananchi wote, inayofuatwa na Chama kwa lengo la kuharakisha maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kuamini na kutegemea uwezo na akili ya kila mwanadamu aliye huru, na pia matumizi mazuri ya mali asili za nchi, na kwa kuzingatia Haki za Binadamu.

(r) "Viongozi Wakuu wa Kitaifa" ina maana ya Mwenyekiti wa Taifa, Makamu Mwenyekiti na Katibu Mkuu wa Chama.

(s) "Viongozi wa Kitaifa" ina maana ya Manaibu Katibu Mkuu, Wajumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la Taifa, Wakurugenzi na Manaibu Wakurugenzi wa Chama katika ngazi ya Taifa, wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Chama.

(t) "Kiongozi wa Serikali" ni pamoja na:-

(i) Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano atokanaye na Chama.

(ii) Rais wa Zanzibar na Makamu wa Rais wa Zanzibar atokanaye na Chama.

(iii) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano

(iv) Waziri atokanaye na Chama

(v) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atokanaye na Chama.

(vi) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar atokanaye na Chama.

(vii) Spika wa Bunge na Spika wa Baraza la Wawakilishi atokanaye na Chama.

(viii) Diwani na Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya au Mji atokanaye na Chama.

(ix) Kiongozi wa serikali ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa atokanaye na Chama.

(u) "Walinzi wa Chama" ni vijana wa kike na wa kiume wasiokuwa na silaha, waliojitolea kwa hiari yao pasina malipo yoyote kulinda na kuweka usalama wa Viongozi Wakuu, Viongozi wa Kitaifa na viongozi wengine wa Chama pamoja na mali za Chama, majengo ya Chama, kulinda mikutano ya Chama ifanyike kwa salama na amani, na shughuli nyingine za Chama ambapo walinzi hao watajulikana kwa jina la Blue Guards". Walinzi hawa wa Chama hawaruhusiwi kuchukua au kuwa na silaha ya aina yoyote wakati wa kufanya shughuli za Ulinzi wa Chama na mali zake.

(v) "Kutunga" ni pamoja na kufuta, kurekebisha, kubadilisha Katiba hii, ama kuongeza au kupunguza sehemu ya/au Kifungu cha, au vifungu vya Katiba hii pamoja na kutunga Kanuni, kuzifanyia marekebisho, kuzifuta na kuweka Kanuni mpya.

(w) Kila inapotajwa moja itafsiriwe kama ni wingi na kila penye wingi itafsiriwe vile vile kama ni moja.

(x) Kila penye neno la uke lisomwe pamoja na neno la uume na hivyo kila penye neno la ume pasomeke na neno la uke.

(y) Kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya kazi fulani kwa kutaja madaraka ya kazi yake ifahamike kuwa mtu anayehusika ni pamoja na mtu yeyote yule anayekaimu au aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kushikilia dhamana ya kazi hiyo.

Utekelezaji wa vifungu mbali mbali

126. Utekelezaji wa masharti ya vifungu mbali mbali vya Katiba hii vinavyohusu marekebisho ya uchaguzi na, au uteuzi wa wajumbe wa vikao vya Chama katika ngazi mbali mbali hautoathiri uchaguzi na, au uteuzi ambao umekwishafanyika katika uchaguzi wa Chama ndani ya Chama uliokwisha malizika wakati marekebisho haya yanapitishwa.

Jina la Katiba, kuanza kutumika na uhakiki wa yaliyofanywa

127. (1) Jina la Katiba hii ni Katiba ya The Civic United Front (CUF – Chama cha Wananchi 1992) Toleo la 2014, na kwa kiingereza " The Constitution of the Civic United Front (CUF – Chama cha Wananchi1992) 2014 Edition.

(2) Katiba hii itaanza kutumika kuanzia tarehe 22 Agost 2014.

(3) Jambo lolote lililofanywa au kutokufanywa chini ya Katiba ya zamani kwa misingi ya matakwa ya Katiba hiyo, litaendelea kuwa halali chini ya Katiba hii mpaka pale ambapo jambo hilo au kitendo hicho kitakapokuwa kimerekebishwa au kubadilishwa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba hii, na kwamba uteuzi uchaguzi, uamuzi au maelekezo mengine yoyote yaliyofanywa chini ya Katiba ya zamani bado yatakuwa na nguvu za kikatiba hadi pale uteuzi au uchaguzi mwengine au uamuzi mwengine au maelekezo mengine yoyote yatakapokuwa yamefanywa au yametolewa chini ya matakwa ya Katiba hii mpya.

(4) Kanuni zozote zilizotungwa chini ya Katiba ya zamani zitaendelea kutumika, na zitakuwa halali na zenye nguvu kamili kama kwamba zimetungwa chini ya Katiba hii mpaka pale kanuni hizo zitaporekebishwa au kubadilishwa kwa mujibu wa matakwa ya Katiba hii mpya.

NYONGEZA YA KWANZA

BENDERA YA CHAMA

(Imetajwa katika kifungu cha 2 cha sura ya kwanza ya Katiba hii)



NYONGEZA YA PILI

WIMBO WA TAIFA WA CHAMA

(Imetajwa katika kifungu cha 4(1) cha sura ya kwanza ya Katiba hii)

(1) CUF-Chama cha Wananchi,
Mlinzi nayo chemichemi,
Ya haki za Wananchi,
Bara nako Visiwani .

(2) Siasa itumikie,
Uchumi wa nchi yetu,
Ni mwiko huo uchumi,
Kutumikia siasa.

Ni HAKI SAWA
Kwa watu wote,
Kuendeleza Taifa letu,
Utajirisho itikadi yetu,
Tukatae kuonewa x 2

CUF